Haliuzwi
NOVEMBA 17, 2025
/islamicftz
Jumada I 26 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 558
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## Mitihani kidato cha nne kuanza leo, 311,986 waachia ngazi njiani

# Misk ya Roho: ilipotoka hadi sasa



MASHEIKH WATAKAONOGESHA MISK YA ROHO 2025 JIJINI DAR

Sheikh Hassan Muhammadayn
Sheikh Abdallah AbdulQadir Al-Ahdal
Sheikh Aboubakar Misigaro
Sheikh Abdulkhaaliq Issa
Sheikh Twalib Hassan
Sheikh Hassan Abdushakuur

■ Misk ya Roho 2025 inarejea baada ya kutofanyika kwa miaka 5 Mwenyekiti TIF, Aref Nahdi, akitaja sababu kuu kuwa ni uhaba wa fedha, ingawa katika miaka hiyo ugonjwa wa Corona pia uliibuka na kutikisa dunia.

# Rais Samia, Mwinyi waanza kuliponya taifa



"Namwomba Mwenyezi Mungu, mwisho wa utumishi wa awamu ya sita usipimwe tu kwa vitu vitakavyoachwa, bali tupimwe kwa tabasamu tutakaloliacha kwenye nyuso za Watanzania." Rais Samia Suluhu Hassan



## Kwa nini hatua ya Samia kuanzisha Wizara ya Vijana ni muhimu na mwafaka

## Viongozi wa Kiislamu wakemea wahalifu waliochochea vurugu

## Mwinyi atema nyongo akitoa mwelekeo mpya utendaji kazi mawaziri

## Hadhi ya Qur'an ilindwe katika viapo serikalini

# Misk ya Roho: Ilipoanza hadi sasa

**Kama jina linavyodokeza Misk ya Roho iliacha athari chanya ya harufu kwenye roho za watu wengi. Hili ni jukwaa ambalo lilikusanya masheikh wabobevu katika da'awah kutoka nchi zaidi ya tano za Afrika ya Mashariki wenye uzoefu mkubwa.**

Historia ya Misk ya Roho inaanza takriban miaka 10 iliyopita pale Kongamano la Kimataifa la Kidaawah lilipofanyika pale katika ukumbi wa Diamond Jubilee mwaka 2016 huku Mufti Ismail Menk wa Zimbabwe akikaribishwa kama mzungumzaji mkuu.

Baada ya kongamano, watu wengi walipongeza juhudi za kumleta mgeni mkubwa kama Muft Menk lakini pia wakataja kuwa lugha imekuwa kikwazo kwa wengi. Watu wakashauri kuwepo kwa tamasha au kongamano la Kimataifa kwa lugha ya Kiswahili.

Taasisi ya The Islamic Foundation, kama kawaida yake, imekuwa sikivu mno kwa wadau wake. Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi, akaita makamanda wake na kuwataka kuchakata wazo hilo na kuja na mpango utakaokata kiu ya wapenzi wa da'awah.

Hapo ndipo wazo la Misk ya Roho lilipozaliwa, kama ambavyo Mkurugenzi wa Matamasha wa taasisi hiyo Limbanga Mohamed Limbanga alielezea katika mahojiano maalum yaliyofanyika studio za TV Imaan wiki iliyopita, alipoamsindikiza Mwenyekiti kuzindua Misk ya Roho 2025.

Misk ya Roho 2025 inarejea baada ya kutofanyika kwa miaka 5 Mwenyekiti akitaja sababu kuu kuwa ni uhaba wa fedha, ingawa katika miaka hiyo ugonjwa wa Corona pia uliibuka na kutikisa dunia.

Akitania, Nahdi pia alisema taasisi yake ilitaka kuwapima Waislamu kama wana subira, na bila shaka amethibitisha subira ya watu.

## Misk ya Roho ni nini?

Limbaga alitoa maana ya kutosheleza ya chapa hii, kuwa ni kongamano la Afrika ya Mashariki kwa lugha ya Kiswwahili ambalo linawakutanisha masheikh kutoka eneo hili la Afrika kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa jamii.

Kama nilivyodokeza ilipoonekana haja ya kuanzishwa kwa kongamano hilo, maandalizi yakafanyika.

Mwaka 2017 kwa mara ya kwanza, kongamano hilo lilifanyika, mada kuu ikiwa ni "Jinsi ya kuwa na Ikhlaas, umuhimu wa elimu na thamani ya amani."

Miongoni mwa masheikh waliohudhurisha mada katika kongamano hilo la kwanza la kihistoria la Misk ya Roho walikuwa ni pamoja na Sheikh Nurdin Kishk na Sheikh Salim Barahiyan kutoka Tanzania, Sheikh Juma Amir na Sheikh Yusuf Abdi wa Kenya, Jamal Maboyi wa Rwanda, Sheikh Ibrahim Kyebanja wa Uganda na Sheikh Zuberi Bizimana wa Burundi.

Katika kongamano lile Omar Muhammad, mtoto mdogo wa Kenya aliyejipata umaarufu kwa kumlimgania Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta ili awe Muislamu pia alikuwepo. Omar Muhammad kijana aliyemlingania Rais Kenyatta wa Kenyatta awe Muislamu.

Wageni mashukuri walioweka historia kwa kuhudhuria kongamano lile la kihistoria ni pamoja na Muft na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zubeir; Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi na Rais wa taasisi ya Alhikma Foundation, Sheikh AbdulQadir bin Muhammad Ahmad al-Ahdal.

Ukumbi wa Diamond Jubilee ulfurika watu, wakafurahi mno. Maombi ya watu yakapokelewa yakitaka kongamano lile liwe endelevu kwa kufanyika kila mwaka.

Na kweli, bila khiyana, mwaka uliofuata 2018, likafanyika tena kongamano hilo mada kuu ikiwa ni "Utukufu Wake" huku baadhi ya masheikh walioshirikishwa katika kutoa mhadhara wakiwa ni pamoja na kutoka Tanzania, Sheikh Dur Mohammed Issa na Sheikh Ally Jumane huku Kenya ikiwakilishwa na Sheikh Yusuf Abdi na Sheikh Jamaldin Osman. Wengine na nchi wal-





izotoka ni pamoja na Sheikh Zubeir Bizimana wa Burundi, Sheikh Ally Kajura wa Rwanda na Sheikh Mohammad Abduely wa Uganda.

Likafuata kongamano la tatu lililobeba mada kuu ya Kitabu changu ambapo Sheikh Ibrahim Twaha ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa The Islamic Foundation na Sheikh Salim Qahtwani kutoka Tanzania walikuwa ni miongoni mwa walinganiaji waliohudhurisha mada. Kutoka Kenya, kwa mara ya tatu mfululizo, Sheikh Yusuf Abdi alikuwepo pamoja na Sheikh Abuu Hamza huku kutoka Uganda Sheikh Mohammed Abdulely akirejea kwa mara ya pili mfululizo na kutoka Rwanda ni Sheikh Djumapili Mbabajende.

Kutokana na changamoto mbalimbali, baada ya mwaka huo kongamano lilisimama kwa miaka mitano.

Baada ya kusimama, maombi mengi yaliendelea kupokelewa kila mwaka kuhitaji kongamano hili. Wapenzi wake wakilalamika na kukumbusha– Mnaturejeshea lini kongamano letu.

Hata hivyo, hali hii ya kiu kubwa ya kuona kongamano linarejea inaeleweka hasa kwa anayejua maana ya kongamano hili na athari pana na za kina ambazo limezalisha katika ile miaka mitatu ya mwanzo.

## Athari ya Misk ya Roho

Kama jina linavyodokeza Misk ya Roho iliacha athari chanya ya harufu kwenye roho za watu wengi.

Hili ni jukwaa ambalo lilikusanya masheikh wabobevu katika da'awah kutoka nchi zaidi ya tano za Afrika ya Mashariki wenye uzoefu mkubwa. Kwa hiyo wahudhuriaji, walitoka wakiwa wameshiba maarifa ya dini katika kutengeneza mustakabali mwema wa dunia na akhera yao.

Ukiacha mhadhara mkuu aghlabu kumekuwa na khutba au/na mihadhara midogo ya utangulizi au ya baada ya kongamano, ambayo aghlab ililenga makundi maalum na kutoa elimu ya juu sana katika eneo mahsusi.

Ikumbukwe, athari ya makongamano haya haikuishia kwa watu elfu 5 hadi 6 waliokuwepo ukumbini bali ilienea eneo lote la Afrika ya Mashariki na kufikia mamilioni ya watu, kupitia vyombo vya habari hususan TV, redio, mitandao ya kijamii vilivyorusha moja kwa moja au kwa kwa kurekodi au kwa maandishi.

Sina shaka, jukwaa hili la kuwasilisha Uislamu katika uhalisia wake – kama dini bora ambayo Allah amewachagulia wanadamu - limechangia watu kusilimu, limewavuta Waislamu kuwa hai tena na muhimu lilichangia mno amani ya nchi, ambayo imekuwa ikihubiriwa mara zote.

Kwa masheikh wenyewe, kongamano hili limekuwa fursa adhimu ya kukutana, kujuana kiundani na kubadilishana uzoefu katika kazi ya da'awah.

Kwa wahudhuriaji, hii nayo imekuwa fursa adhimu kutengeneza mtandao wa marafiki (networking) wanaoweza kusaidiana katika nyanja mbalimbali za kimaisha, kama ambavyo Limbanga anakiri makongamano yamempa marafiki wanaomfaa hadi leo.

Kwa baadhi, katika dunia hii ambayo sehemu za kheri ambapo Waislamu kutembelea na kupumzisha akili ni chache, kongamano la Misk ya Roho limekuwa ni mtoko wa maana wa kifamilia. Na bahati nzuri, waandaaji wamekuwa wakijitahidi sana kuhakikisha mazingira ni rafiki - kuanzia mapambo ya huduma za ukumbini, chakula, mahali pa kusalia, ulinzi na mengineyo.

## Habari njema – Misk ya Roho imerejea

Mwenyekiti Aref Nahdi wa The Islamic Foundation hatimaye kasikiliza watu na karejesha kongamano hili pendwa.

Jumamosi ya Desemba 27, 2025 pale Diamond Jubilee saa 2 hadi saa 10 alasiri, watu 5,000 watakongamana kwa ajili ya Misk ya Roho, inshaAllah.

Tunapenda sana watoto lakini chini ya miaka 10 usiwabebe ili kujenga hali ya utuivu ukumbini. Kiingilio ni Tsh 15,000/= tu na hii kama Nahdi alivyosema, imewekwa ili kuzoeshana kuchangia dini ya Mwenyezi Mungu.

Ikumbukwe makadirio ya gharama zote za kuandaa shughuli hii ni zaidi ya Milioni 180 na wawezeshaji ni sisi, kwa kadri ya uwezo wa kila mmoja wetu. Kwa wafanyabiashara hii ni fursa adhimu ya kutakasa mali yako kwa kuchangia dini ya Mwenyezi Mungu.



NA MWANDISHI WETU



# Rais Samia aanza kuliponya taifa

Siku 17 tu baada ya uchaguzi ulioambatana na uhalifu uliochochewa na wanasiasa na wanaharati husuan wanaoishi ughaibuni, taswira mpya ya uongozi imeanza kuchongwa upande wa Bara na Visiwani huku msisitizo ukiwekwa katika maridhiano ya kisiasa.

Huko Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan ametumia ufunguzi wa Bunge la 13 kama jukwaa la kusimika ajenda ya maridhiano, amani na Katiba mpya, huku akiweka wazi kuwa Serikali yake haitavumilia uzembe katika utendaji.

Wakati huohuo, Ikulu Zanzibar, Rais Dkt Hussein Mwinyi ametangaza "vita mpya ya kazi", akipanua baraza lake la mawaziri na kuonya kuwa safari hii atakuwa mkali zaidi katika kusimamia uwajibikaji.

Kwa pamoja, kauli zao tangazo la nia yao katika ujenzi wa muafaka wa kitaifa, kupambana na wazembe, wala rushwa na wanaotumia madaraka vibaya sambamba na kuimarisha amani, umoja wa nchi na kufufua mchakato wa Katiba mpya kunatoa matumaini zaidi kwa Watanzania na Jumuiya ya Kimataifa.

## Safari ya maridhiano

Akizungumza bungeni jijini Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan ameelezea kuhuzunishwa kwake na vurugu zilizotokea wakati wa uchaguzi mkuu wa Oktoba 29, 2025. Alisema ili kuzuia tukio hilo kujirudia tena, ataunda tume maalumu kuchunguza chanzo cha machafuko ikiwa ni msingi wa maridhiano.

Hatua hiyo, inaipa sura ya kitaasisi falsafa ya R4 aliyoibeba katika muhula wake wa kwanza – ya kuunganisha Taifa kupitia maridhiano, mageuzi, maelewano na maendeleo. Samia alisisitiza kwamba maridhiano si udhaifu, bali ni uwekezaji katika amani ya siku zijazo.

Awali, wakati anaanza hotuba yake, aliomba waheshimiwa wabunge na taifa kwa jumla, wasimame kwa dakika moja kuwaombea waliopoteza maisha kutokana na vurugu hizo na majeruhi wote wapate nafuu haraka ili warejee katika majukumu yao ya kawaida.

Pia, aliwaomba waliopoteza mali zao kuwa na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu na kusisitiza kuwa Serikali inafanya kila iwezalo kuhakikisha Tanzania inarejea kwenye "utulivu, haki na umoja".

## Vijana sasa kipaumbele

Sehemu iliyoigusa sana jamii, hususan vijana, ni tangazo la msamaha kwa wale waliofikishwa mahakamani kwa mashitaka ya uhaini kwa kufuata mkumbo wa vurugu na maandamano. Zaidi ya watu 500 – wengi wao vijana – wamefikishwa mahakamani kutokana na matukio ya Oktoba 29.

Rais Samia, akijitambulisha kama "mama na mlezi wa Taifa", aliiagiza Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuchunguza upya kesi hizo na kuangalia ni vijana gani "waliofuata mkumbo" bila dhamira ya kufanya uhalifu, ili makosa yao yafutiwe.

Wito wake kwa vijana ulikuwa wa moja kwa moja: nchi hii imejengwa kwenye misingi ya amani, na kizazi kipya kisikubali kushawishiwa kuivuruga. Ameonya dhidi ya "kukata tawi la mti mlilolikalia" na kuwakumbusha kuwa wao ndio walinzi na wajenzi wa Taifa, si wabomoaji wake.

Zaidi ya msamaha, hatua nyingine inayolenga kurejesha imani ya vijana ni kuanzishwa kwa Wizara kamili ya Vijana ndani ya Ofisi ya Rais, badala ya kuwa idara kwenye wizara yenye majukumu mengi. Pamoja na hilo, ameeleza mpango wa kuwa na washauri maalumu wa masuala ya vijana ndani ya Ikulu, ili sauti zao zisipotee kwenye kelele za siasa na urasimu.

Hii yote inaashiria kutambua kwamba kundi linalolalamika zaidi – vijana wasio na ajira, wanaohisi kutosikilizwa na wanaohisi mfumo

# Rais Samia aanza kuliponya taifa



wa kisiasa unawapuuza – linahitaji majibu ya sera, si maneno pekee.

## Katiba mpya na kuijenga upya imani ya kisiasa

Moja ya maeneo ambayo yamekuwa kilio cha muda mrefu kwa sehemu kubwa ya wananchi, hususan vijana, wanaharakati na vyama vya siasa, ni mchakato wa Katiba mpya.

Rais Samia ametumia ilani ya CCM 2025–2030 kama ngao ya kisiasa kutangaza kwamba Serikali itaanza kulifanyia kazi suala la mabadiliko ya Katiba ndani ya siku 100 za muhula wake wa pili. Hatua ya kwanza itakuwa kuanzishwa kwa Tume ya Usuluhishi na Maelewano, ambayo itatazama namna bora ya kulifufua ajenda hiyo kwa njia shirikishi.

Amekiri hadharani kwamba dola linajifunza kutokana na mapito yake; kwamba demokrasia ya Tanzania imekomaa kwa uzoefu, lakini bado inahitaji kuboreshwa kwa kuzingatia "tamaduni, mila na desturi zetu, si za kuletewa".

Kwa waliokatishwa tamaa na kusuasua kwa mchakato wa Katiba mpya katika kipindi kilichopita, kauli hii inaonekana kama mlango mpya wa matumaini.

## Uchapakazi, rushwa na ujumbe kwa watumishi wa umma

Mbali na maridhiano, Rais Samia ametuma pia ujumbe mzito kwa watendaji wa Serikali: ama mwende na kasi ya mabadiliko, au "tutawabadilikia".

Amesisitiza kwamba ahadi za chama chake ni nyingi, matarajio ya wananchi ni makubwa na muda wa utekelezaji ni mfupi. Hivyo hakuna nafasi kwa uvivu, urasimu na ukiritimba unaochelewesha maendeleo. Viongozi kuanzia mawaziri, wakuu wa mikoa, wilaya hadi ngazi ya kata na tarafa, wametakiwa kuwa karibu na wananchi, kusikiliza changamoto zao na kuonesha matokeo.

Ndani ya kauli hii kunasikika pia ujumbe mpana kuhusu mapambano ya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Uzembe, kificho cha taarifa, ulaji wa fedha za miradi na "mikataba hewa" mara nyingi hujificha kwenye visingizio vya michakato.

# Wengi waunga mkono ramani ya mageuzi ya kiuchumi

Rais Samia Suluhu Hassan ameahidi kuwa Serikali ya awamu ya sita katika muhula wake wa pili itaendeleza mageuzi ya kiuchumi kwa kuipa kipaumbele sekta binafsi, kuwekeza zaidi kwenye kilimo na kuimarisha huduma za afya na elimu.

Akizindua Bunge la 13 jijini Dodoma, Rais Samia alisema Serikali itaendelea kuitambua sekta binafsi kama mhimili wa ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi kwa kuboresha mazingira ya biashara kupitia kukamilisha mpango wa kuboresha mazingira hayo na kutekeleza mapendekezo ya tume ya maboresho ya mifumo ya kodi ili kuwapa wafanyabiashara urahisi wa kufanya biashara.

Kufuatia houba hiyo uchunguzi wa gazeti hili umeonesha wananchi wengi wamevutiwa na mipango ya Rais Samia na wanaamini kuwa Tanzania itafika mbali kwani ameshathibitisha uwezo wa kuivusha nchi katika ngwe ya kwanza.

Katika aliyoahidi Rais Sami ani pamoja na kuweka nguvu katika kudhibiti mfumuko wa bei ili kupunguza gharama za maisha, pamoja na kutoa motisha kwa viwanda vya ndani kuzalisha kwa gharama nafuu na kuuza ndani na nje ya nchi. Aidha, vikwazo vya kikodi na visivyo vya kikodi vitaondolewa ili kuchochea uzalishaji na kuongeza ushindani wa bidhaa za ndani.

Akizungumzia ajira na ustawi wa vijana, Rais Samia alisema Serikali itafungua fursa maalumu za kuwawezesha vijana na wamiliki wa biashara ndogondogo kupata elimu ya biashara na kuwasaidia kujisajili kwenye mfumo wa manunuzi ya umma wa kielektroniki. Kupitia vyuo vya ufundi stadi, Serikali itaongeza programu za mafunzo zinazounganishwa na miradi ya kimkakati kama reli ya kisasa, bandari, uchumi wa buluu, madini na gesi ili vijana wapate uzoefu na ujuzi wa kuajirika.

Alisema pia zitaanzishwa kanda za kuendeleza ujuzi ili kukidhi mahitaji ya kampuni za sekta binafsi, pamoja na kuangalia vivutio maalumu kwa kampuni zitakazotoa ajira nyingi kwa vijana. Vyuo vitahimizwa kutoa mafunzo ya ulezi na ukuzaji wa viongozi vijana, huku matarajio yake yakiwa kwamba ifikapo 2030 Tanzania iwe na wawekezaji vijana wanaotoa ajira kwa wenzao.

Katika sekta ya kilimo, Rais Samia alisema Serikali itaongozwa na kauli mbiu "kilimo ni biashara, mkulima ni mwekezaji," ikilenga kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta hiyo kutoka asilimia 4 hadi 10 ifikapo 2030. Alisema dhamira ni kujihakikishia usalama wa chakula na kuwekeza kwenye mnyororo wa thamani, huku Tanzania ikilenga kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa mahindi, mchele na mbogamboga barani Afrika.

Amesema Serikali itaongeza upatikanaji wa pembejeo kwa ruzuku, kupanua umwagiliaji kutoka ekari milioni 3.4 hadi milioni 5 kwa kukamilisha mabwawa na skimu zinazoendelea na kuanzisha mpya katika Bonde la Rufiji, kuanzisha vituo vya ukodishaji zana za kilimo na kuziimarisha TADB na Benki ya Ushirika ili kuchochea uwekezaji.

Kuhusu ajira kwenye huduma za jamii, Rais Samia alieleza kuwa ndani ya siku 12 tangu aapishwe kwa muhula wa pili tayari ametangaza ajira 7,000 za walimu na 5,000 za watumishi wa afya, akisema ni mwanzo wa kuboresha huduma hizo.

Pia amesema Serikali inajiandaa kuanza majaribio ya Bima ya Afya kwa Wote, kuviunganisha vituo vya kutolea huduma za afya kidijitali na kuweka viwango vinavyofanana ili watumiaji wa bima vijijini na mijini wapate huduma zinazolingana. Ameielekeza Wizara ya Afya kusimamia maagizo ya kutokuzuia maiti hospitalini wakati familia zikiendelea na taratibu za ulipaji deni kwa njia zinazolinda utu, na amewataka wananchi kuweka kipaumbele afya zao kwa kuwa na bima ya afya wao na wategemezi wao.

NA MWANDISHI WETU



# Rais Mwinyi atema nyongo akitoa mwelekeo mpya utendaji kazi mawaziri

Wakati Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi akiwaapisha mawaziri aliowateua amesema siyo wakati wa kwenda kufanya sherehe badala yake ni muda wa kujitathmini, kutafakari namna gani watakidhi matakwa ya wananchi.

Katika kuliendea hilo aliwatwisha zigo la mambo 12 mbayo wanatakiwa kuyafanyia kazi kwa kasi zaidi ili kuleta mabadiliko katika kipindi cha pili cha utawala wake kama Rais wa visiwa hivyo maarufu kwa utalii na uzalishaji wa karafuu.

"Kuna mawaziri wapya lakini wengi mlikuwapo, kuanzia sasa tutawapima nimeshawaambia tunataka kasi zaidi ya ile ya kipindi kilichopita, huu siyo wakati wa sherehe bali nendeni mkatafakari na kujitathmini namna ya kukidhi matakwa ya wananchi, alisema Dk Mwinyi akiwaapisha jana, Ikulu Zanzibar.

Mbali na kutoa maagizo hayo, pia Rais Mwinyi alikiomba Chama cha ACT-Wazalendo kuona umuhimu wa kuunganisha nchi na watu wake kwa kuingia ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

"Tumeacha nafasi za wizara nne ili kuwasubiria wenzetu ambalo ni takwa kikatiba, naendelea kuwaomba waone umuhimu wa kuunganisha nchi na watu wake ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa," alisema Dk Mwinyi.

Kwa nyakati tofauti tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu Oktoba 29, Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Othman Masoud katika mikutano ya kuwashukuru wananchi kisiwani Pemba amekuwa akisema kipaumbele chao kwa sasa siyo kuingia SUK bali ni kuangalia namna ya kushughulikia changamoto zilizojitokeza wakati wa uchaguzi kwa madai ulikuwa uchaguzi ambao haukuwa na haki.

Alisema kwa sasa wanaangalia namna ya kwenda mahakamani kupinga ushindi huo. Hata hivyo kwa mujibu wa katiba na sheria za Zanzibar matokeo ya Rais hayapingwi mahakamani isipokuwa ya uwakilishi na ubunge.

## Maagizo kwa mawaziri

Dk Mwinyi aliwataka mawaziri hao kuwa wabunifu kushughulikia changamoto za wananchi kwa kuwafuata kwenye maeneo yao badala ya kukaa ofisini.

Kiongozi huyo amesema katika kipindi kilichopita mawaziri walikuwa wakimpelekea changamoto zote yeye azishughulikie.

"Changamoto msinipe mimi, nimewateua mnisaidie sasa inakuwa haina maana kuniletea tena changamoto zote kwangu," alisema.

Hata hivyo, aliwaeleza iwapo wakiona mambo yanakuwa magumu kuliko uwezo wao wasikae kimya wakamweleze au wamfuate Makamu wa Pili wa Rais ili kupata ufumbuzi wa haraka.

Jambo jingine, Dk Mwinyi aliwataka mawaziri hao kufanya mabadiliko ya sheria ambazo wanaona ni kikwazo katika utendaji kazi kwani katika kipindi kilichopita wapo baadhi yao ambao wamekuwa wakieleza shida ya sheria ilhali wana uwezo wa kufanya marekebisho barazani.

"Tusiwe watumwa wa sheria zetu, hili nawataka mkalifanye haraka sana iwezekanavyo," alisema.

Dk Mwinyi alisema katika kipindi hiki watakuwa na mkataba nao wa kupima ufanisi na utendaji kazi wao ili kuona kasi ya utendaji kazi wao.

"Wekeni taratibu za utekelezaji wa kazi zenu kila robo mwaka kuonesha mliyofanya," alisisitiza.

Katika kulitekeleza hilo pia Dk Mwinyi aliwataka mawaziri hao kuwa na utaratibu wa kuzungumza na waandishi wa habari kila mara ili kueleza mafanikio na changamoto na namna ya kuzitatua.

"Wapo mawaziri ambao hawapendi kuzungumza na waandishi wa habari, hili sitaki kulisikia lazima muwe tayari kuzungumza kueleza mafanikio na changamoto na jinsi mnavyokwenda kuzitatua," alisema Dk Mwinyi.

جمادى أول

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Mitihani kidato cha nne kuanza leo, 311,986 waachia ngazi njiani

Wanafunzi 595,816 wanatarajia kuanza mtihani wa kumaliza elimu ya sekondari kuanzia leo, wakikamilisha safari yao ya miaka minne.

Idadi hiyo ya watahiniwa ni sawa na asilimia 65.63 ya wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022 waliokuwa 907,802.

Hiyo ikiwa na maana kuwa wanafunzi 311,986 hawakuweza kusajiliwa kufanya mtihani huo kwa sababu ambazo hazijawekwa bayana.

Hali kama hiyo pia ilijitokeza wakati Baraza la Mitihani Tanzania (Necta) lilipotangaza matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2024.

Necta ilisema jumla ya watahiniwa 557,706 walisajiliwa kufanya mtihani huo.

Hata hivyo, uchunguzi wa Mwananchi ulibaini mwaka 2021 wanafunzi hao walipojiunga kidato cha kwanza walikuwa 759,706.

Taarifa iliyotolewa na Tamisemi ilionyesha, wanafunzi 759,706 sawa na asilimia 91.1 kati ya wanafunzi 759,737 waliokuwa na sifa za kujiunga na kidato cha kwanza, walichaguliwa mwaka 2021.

Aidha, wanafunzi 128, 700 pia walipotea katika mtihani wa mwaka 2023 kwani waliofanya walikuwa 572, 338 kati ya 701,038 waliocanguliwa kidato cha kwanza mwaka 2020.

Kama ilivyoulizwa walipo wanafunzi 201,910 walioanza kidato cha kwanza mwaka 2021 na kutakiwa kumaliza mwaka 2024, swali jingine ni walipo wanafunzi 309,986 waliochaguliwa kidato cha kwanza mwaka 2022 na kutakiwa kumaliza mwaka huu.

## Watahiniwa 2025

Jana, taarifa iliyotolewa na Katibu Mtendaji wa Necta, Profesa Said Mohammed, ilieleza idadi ya watahiniwa wa mwaka huu ni ongezeko la asilimia 7.67 ikilinganisha na mwaka 2024.

Watahiniwa hao wanatoka katika jumla ya shule za sekondari 5,868 na vituo vya watahiniwa wa kujitegemea 813, kati yao 569,914 ni watahiniwa wa shule na 25,902 ni watahiniwa wa kujitegemea.

Kati ya watahiniwa wa shule 569,914 waliosajiliwa mwaka 2025, wavulana ni 266,028 sawa na asilimia 46.68 na wasichana ni 303,886 sawa na asilimia 53.32.

"Pia wapo watahiniwa wa shule 1,128 wenye mahitaji maalumu ambapo kati yao, wenye uoni hafifu ni 860, wasioona ni 70, uziwi ni 58, wenye ulemavu wa akili ni 05, na wenye ulemavu wa viungo ni 135," alisema.

Kati ya watahiniwa wa kujitegemea 25,902 waliosajiliwa, wavulana ni 10,862 sawa na asilimia 41.93 na wasichana ni 15,040 sawa na asilimia 58.07.

"Pia katika watahiniwa wa kujitegemea wapo wenye mahitaji maalumu 56. Kati yao, wenye uoni hafifu ni 49 na wasioona," alisema Mohammed.

## Wizara yatoa kauli

Akizungumzia suala hilo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Caroline Nombo alisema ili kuondoa mkanganyiko ulipo, wanataka kutengeneza mfumo mzuri wa kukusanya takwimu ili kuondoa mkanganyiko uliopo sasa.

Alisema kuwa mfumo huo pia utasaidia kufanya ufuatiliaji wa wanafunzi tangu anapoanza chekechea shule yoyote iwe shule ya kiingereza, kimataifa au Serikali ili kurahishisha kujua wanafunzi wako wapi na wanafanya nini.

"Sitaki kuamini kuna mdondoko kwa kiasinm hiki tunatakiwa kuthibitisha hizi takwimu, lakini kupitia mfumo huu tutaweza kujua kwani tunatambua kuna wengine wanakariri wengine wanahama nchini lazima tuzithibitishe, hata akienda mfumo wowote lazima tujue," alisema Profesa Nombo.

Alisema ujio wa namba ya jamii itakayokuwa ikisajili watoto tangu wanapozaliwa, pia itakuwa na mchango chanya katika kurahisisha ufuatiliaji wa wanafunzi tangu wanaaandikishwa shule ili kusaidia kujua wanatoka wapi wanakwenda wapi.

"Lakini hata wanaoondooka, Serikali imeweka nafasi ya wao kurudi tena shuleni na wapo wengi waliorudi katika mfumo usio rasmi na wengine wamerudi katika mfumo rasmi, wengi wamerudi na wengine wameenda hata vyuo," alisema.

Alieleza kuwa Serikali pia inasaidiana na jamii ili kuhakikisha watoto wanaandikishwa shule, kufuatilia maendeleo yao kwa kuhakikisha vijana wanakwenda shule, wanabaki shule huku wakitengenezewa mazingira mazuri.



Katibu Mtendaji wa Necta, Profesa Said Mohammed

جمادى أول

HABARI DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU



# Viongozi wa Kiislamu wakemea wahalifu waliochochea vurugu Okt 29

Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata), kupitia Baraza la Ulamaa, limelaani vikali matukio ya uhalifu na vurugu zilizotokea Oktoba 29, 2025 na kusababisha vifo, majeruhi na uharibifu mkubwa wa mali za umma na binafsi, likiitaka Serikali kufanya uchunguzi wa kina kubaini vinara wa vurugu hizo.

Katika tamko lililotolewa Novemba 13, 2025 na kusainiwa na Katibu wa Baraza la Ulamaa, Sheikh Hassan Chizenga, Bakwata limesema limesikitishwa na matokeo ya vurugu zilizojitokeza siku hiyo na kuacha majonzi kwa familia, taasisi na Taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa tamko hilo, siku ya tukio kulizuka kundi la watu waliokuwa wakitisha raia, kupora na kuharibu mali, likivuruga shughuli za kawaida na kushambulia miundombinu mbalimbali ikiwemo vituo vya mafuta, ofisi za umma na ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Baraza hilo limesema vitendo hivyo vilisababisha vyombo vya ulinzi na usalama kuingilia kati kurejesha hali ya utulivu, hatua ambayo ndani yake kulijitokeza vifo vya watu wasiokuwa na hatia, baadhi kupata ulemavu wa kudumu na wengine kupoteza mali kwa wizi na uharibifu.

"Vitendo hivi vya kihalifu vimeleta majonzi makubwa. Wapo waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki, wapo waliopata ulemavu wa kudumu na wapo walioporwa mali zao au kuharibiwa miundombinu yao. Yote haya yamesababishwa na kundi lililokuwa likifanya fujo, wizi na uharibifu mkubwa wa miundombinu," limesisitiza tamko hilo.

Bakwata imeeleza kuwa matokeo ya vurugu hizo yameigawanya jamii katika makundi mawili; wale walioonekana kufurahia na kuchochea uhalifu huo, na wale walioumizwa na kusikitishwa na madhara yaliyotokea, hivyo kuibua hitaji la kuchukua hatua zenye kulinda haki na amani ya Taifa.

Katika hatua ya kwanza, Baraza hilo limeitaka Serikali kufanya uchunguzi wa kina kubaini watu wote waliokuwa vinara wa kuwachochea vijana na makundi mbalimbali kuingia mitaani na kufanya vitendo vya kihalifu vilivyosababisha kupotea kwa maisha ya watu na uharibifu wa mali.

"Tunaiomba Serikali ichunguze kwa kina chanzo na wahusika wakuu wa uhalifu huu, ili sheria ichukue mkondo wake ipasavyo kwa wale waliothibitika kuhusika katika kupanga na kuhamasisha vurugu hizi," limeeleza.

Hata hivyo, pamoja na wito wa kuchukua hatua kali kwa wahalifu, Bakwata imetoa mwito kwa Serikali kuangalia kwa jicho la huruma wale raia ambao wamekumbwa na madhara ya tukio hilo bila kuwa sehemu ya kupanga au kutekeleza uhalifu.

"Tunaisihi Serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma wale wote ambao kwa namna moja au nyingine wameguswa na maafa haya na wala hawakuhusika katika uhalifu... Panapohitajika suluhu, basi ifanyike; panapohitajika msamaha na maridhiano, yafanyike kwa kuzingatia masilahi mapana ya nchi yetu," limeongeza tamko hilo.

Baraza hilo pia limeweka wazi kuwa wito wa suluhu na maridhiano usitafsiriwe kama zawadi kwa wale waliohusika moja kwa moja na uhalifu, bali uwe ni sehemu ya mchakato wa kujenga upya amani na mshikamano wa Taifa huku wahusika wakuu wa uharibifu wakipelekwa kwenye vyombo vya sheria.

"Ingawa tunaisihi Serikali suluhu na maridhiano, isiwe ni zawadi kwa wale wanaohusika kushiriki uhalifu huu uliosababisha maafa. Haki na uwajibikaji viende sambamba na huruma na kujenga umoja wa Kitaifa," linasisitiza tamko la Bakwata.

Tamko hilo limekuja katika kipindi ambacho mjadala wa maridhiano ya Kitaifa na utulivu wa kisiasa umeibuka upya baada ya machafuko ya Oktoba 29, likionesha msimamo wa viongozi wa Kiislamu kwamba amani, umoja na ujenzi wa Taifa lazima viende sambamba na kusimamia sheria, haki na uwajibikaji kwa wote.




# Mabenki ya kidijitali Arabuni yatumia fedha za Kiislamu kujenga imani ya wateja

Mawimbi ya mapinduzi ya benki za kidijitali katika ulimwengu wa Kiarabu yanazidi kupanda, huku taasisi nyingi zikigeukia misingi ya fedha za Kiislamu ili kujenga imani na kuvutia watumiaji wapya, inaeleza makala ya mwandishi Salma Abdelsalam iliyochapishwa na jarida la CairoScene tarehe 15 Novemba 2025.

Kwa miongo mingi, benki katika nchi za Kiarabu zilitambulika kwa majengo makubwa, foleni na karatasi zenye mihuri ya mkono. Sasa taswira hiyo inabadilishwa na mfumo wa mabenki ya kidijitali yanayojengwa juu ya algoriti, ubunifu na skrini za simu, mabadiliko ambayo si ya urahisi pekee bali yanabadilisha namna watu wanavyoshiriki kwenye mifumo ya kifedha na jinsi uchumi unavyojibadilisha.

Kwa mujibu wa Abdelsalam, mageuzi haya yameungwa mkono na kanuni shupavu za udhibiti. Saudi Arabia, kupitia Benki Kuu (SAMA), ilitoa leseni za kwanza za mabenki ya kidijitali mwaka 2022 kwa STC Bank na Saudi Digital Bank kama sehemu ya utekelezaji wa Vision 2030 ya uchumi usioitegemea sana fedha taslimu. Nchini UAE, Wio Bank, Zand na Al Maryah Community Bank zimezinduliwa katika kipindi cha miaka mitatu, zikilenga pengo tofauti kuanzia SMEs hadi vijana wa kizazi cha kidijitali. Bahrain imeendelea kuwa "sandbox" ya fintech kupitia mfumo wa udhibiti unaoruhusu mabenki ya mtandaoni pekee.

Hata katika masoko yaliyozoea mifumo ya zamani kama Misri na Jordan, benki za jadi zinakimbizana na mabadiliko ya kidijitali huku wanaoanza (startups) wakijaribu mifumo ya "wallet-based neobanks". Misri imefikia hatua ya kuidhinisha benki ya kwanza ya kidijitali, onebank (zamani Misr Digital Innovation), iliyo chini ya Banque Misr, huku Telda ikivutia kizazi cha Gen Z kupitia kadi za malipo na zana za kupanga bajeti.

Makala inabainisha kuwa nguvu kubwa ya mabadiliko haya ni idadi ya vijana: karibu asilimia 60 ya wakazi wa MENA wako chini ya miaka 30, na penetrasheni ya simu janja inazidi asilimia 90 katika masoko ya Ghuba. Hawa wanahitaji huduma za kifedha za haraka, bila matawi, zenye usajili wa papo kwa hapo na usaidizi wa mazungumzo (chat).

## Wanajeshi Waislamu wa Kenya nchini DRC wasaidia msikiti Beni

Wanajeshi Waislamu wa Kikosi cha Haraka cha Kenya (Kenyan Quick Reaction Force 4 – KENQRF 4) wanaohudumu chini ya Ujumbe wa Umoja wa Mataifa wa Kurejesha Amani DR Congo (MONUSCO), wamefanya mchango mkubwa kwa Masjid Riyaadha mjini Beni, wakieleza kuwa ni sehemu ya kuimarisha udugu wa Kiislamu na kusaidia jamii wanayoihudumia.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Ulinzi ya Kenya, mchango huo ulitolewa tarehe 13 Novemba 2025 na ulihusisha mazulia ya kuswalia kwa ajili ya ukumbi wa ibada, taa za sola ili kuboresha upatikanaji wa nishati, pamoja na vyakula mbalimbali kwa Waislamu wa eneo hilo. Pia walitoa msaada wa fedha kusaidia kuufufua mradi wa ujenzi wa msikiti uliokwama.

Aidha, wanajeshi hao waligawa nakala za Msahafu kwa waumini wa msikiti huo, kama njia ya kuimarisha ibada na elimu ya dini katika jamii ya Kiislamu ya Beni.

Katika hafla ya makabidhiano, Kamanda wa Kikosi, Luteni Kanali Simon Seda, alisisitiza umuhimu wa kuishi kwa kuzingatia nguzo tano za Uislamu, akieleza kuwa kutoa sadaka ni miongoni mwa matendo yanayoonesha imani ya kweli na kuimarisha uhusiano kati ya taasisi na jamii inayowazunguka. Aliongeza kuwa kusaidiana kunadhihirisha mafundisho ya umoja, ukarimu na huruma katika Uislamu, pamoja na kumtegemea Allah katika jitihada za pamoja za kuleta amani.

## Wasafiri wapitao Saudi Arabia wanufaika na visa maalumu ya Umrah

Wasafiri wa kimataifa wapitao viwanja vya ndege vya Saudi Arabia sasa wanaweza kufanya Umrah kwa urahisi zaidi, kupitia visa mpya ya kusimama njiani (stopover visa) ya saa 96 inayotolewa bure kwa abiria wa ndege za Saudia na Flynas.

Kwa utaratibu huo, msafiri anayesafiri kuelekea Ulaya, Marekani, Afrika au Asia kupitia Saudi Arabia anaweza kubadilisha tu "transit" ya kawaida kuwa ziara fupi ya siku nne mjini Makka na Madina bila kuomba visa ya jadi ya Umrah.

Visa hii ya kusimama njiani hutolewa kwa wasafiri wote wa kimataifa wanaotumia Saudia au Flynas na wanaopita katika Ufalme huo wakiwa njiani kwenda nchi nyingine, ilimradi wawe na pasi halali na tiketi ya kuendelea na safari. Raia na wakazi wa nchi za Ghuba (GCC) pia wanaweza kunufaika na mpango huo. Ingawa visa yenyewe ni bure, wasafiri hulipa ada ndogo ya usimamizi na bima ya afya, na maombi hufanywa mtandaoni moja kwa moja wakati wa kuhifadhi tiketi ya ndege; mara nyingi hukubaliwa ndani ya dakika chache na kutumwa kwa barua pepe.

Ili kufanya Umrah au Ziara ya maeneo matukufu, msafiri anatakiwa kujisajili na kuweka miadi kupitia jukwaa rasmi la Nusuk kabla ya kuingia katika miji mitukufu ya Makkah na Madinah.

Mpango huu ni sehemu ya mkakati wa Vision 2030 wa Saudi Arabia wa kuongeza idadi ya watalii na mahujaji, huku ukiruhusu mamilioni ya wasafiri wanaopita nchini humo kuonja safari ya kiroho bila gharama kubwa na urasimu mrefu wa viza.

MAKALA MAALUM


ABEID OTHMAN

# Hadhi ya Qur'an ilindwe katika shughuli za kiserikali

Hivi karibuni uliibuka mjadala uliogusa hisia za Waislamu, kuhusu kuheshimu Kitabu Kitukufu cha Qur'an katika shughuli za kiserikali, hususan wakati wa kiapo cha wabunge.

Wakati wabunge wakiapa kushika nyadhifa zao bungeni jijini Dodoma, baadhi yao walionekana wakishika Qur'an wakiwa katika mavazi ambayo hayakidhi viwango vya stara, kwa mujibu wa maadili ya Kiislamu.

Wapo walioliona kama jambo la kawaida, lakini kwa wengi ilikuwa ni ishara ya kutozingatiwa heshima ya Qur'an, ambayo ni alama kuu ya Uislamu na mwongozo wa maisha ya Waumini.



Katika Uislamu, Qur'an si kitabu kama vitabu vingine; ni Neno la Mwenyezi Mungu na chanzo cha mwanga wa maisha ya Muislamu.

Kwa msingi huo, inaposhikwa, kusomwa au kutumiwa katika ibada au shughuli maalum kama kiapo, inapaswa kukabiliwa kwa unyenyekevu, usafi na utulivu wa kiroho. Hivyo, kushika Qur'an bila kuwa katika vazi la stara au katika hali isiyo ya usafi inatafsirika kuwa kinyume na mafunzo ya dini na kutokipa heshima Kitabu Kitukufu.

Stara ni nguzo muhimu sana katika maadili ya Kiislamu. Muislamu anatakiwa kuvaa kwa uungwana, unadhifu na heshima, hasa anapofanya ibada au kushika vitu vitukufu vya dini. Mwanaume afunike angalau kutoka kitovu hadi magoti, ilhali mwanamke afunike mwili mzima isipokuwa uso na mikono. Lengo la stara si kufunika mwili tu, bali pia kudhihirisha unyenyekevu, adabu na kujiheshimu.

Anapokuwa katika shughuli nyeti kama kiapo, Muislamu anatakiwa awe katika mavazi yanayoakisi maadili ya dini yake ili kuoanisha imani yake na kitendo anachokifanya. Kushika Qur'an bila stara kunachukuliwa kama kukosa adabu kwa Kitabu Kitukufu na kupuuza uzito wake.

Mbali na suala la stara, usafi wa kimwili pia ni sharti muhimu katika kushika Qur'an. Mafundisho ya Kiislamu yanasisitiza kuwa Muislamu asiguse Qur'an akiwa najisi au katika hali inayomvua hadhi yake ya kiibada.

Usafi unajumuisha kuwa na wudhu, mwili na mavazi safi, na kuepuka hali yoyote inayomfanya mtu kuwa katika najisi kubwa, ndogo au hadathi.

## Ulaji kiapo Tanzania

Katika mfumo wa kisheria wa Tanzania, viongozi wanaoingia madarakani huchagua kiapo kulingana na imani zao. Kwa Waislamu, Qur'an hutumika kama Kitabu Kitakatifu kinachowasimamia mbele ya Mwenyezi Mungu na wananchi.

Kwa sababu hiyo, kitendo cha kula kiapo kina uzito mkubwa wa kiroho na kimaadili.

Kwa msingi huo, kutokana na mjadala ulioibuka Dodoma, kuna haja ya kuweka utaratibu unaoeleweka vizuri kuhusu namna ya kulinda heshima ya Qur'an bila kuvunja haki za watu kushiriki shughuli za kitaifa.

Ni vyema kuwepo maelekezo ya awali kwa wote wanaotarajia kuapa kwa Qur'an ili kuhakikisha wanazingatia stara na usafi wa mwili. Hii itawasaidia kujipanga ipasavyo, bila kuleta taharuki au kuzua mjadala usio wa lazima.

Katika mazingira ambayo mbunge au ofisa hana mavazi yanayokidhi masharti ya stara, mamlaka zinaweza kuweka mavazi mbadala kwa dharura kama vile joho, baibui, shungi na mengineyo yanayoweza kuvaliwa kwa muda mfupi tu wa kiapo. Hii si hatua ya kumdhalilisha mtu, bali ni njia ya kulinda hadhi ya Qur'an na kuondoa taswira inayoweza kuwa ya kudhalilisha Uislamu.

Kwa wale ambao kwa namna yoyote hawaendani na utaratibu huo, inaweza pia kuandaliwa nafasi maalum nje ya ukumbi ambapo kiapo kinaweza kufanyika katika mazingira tulivu na yenye kuzingatia masharti ya dini.

Aidha, ni busara pia kiapo kinachohusisha Qur'an kishuhudiwe na mtu mwenye elimu ya Kiislamu, kama kadhi au sheikh aliyeteuliwa, ili kuhakikisha taratibu zote zinazohitajika zinafuatwa.

Bila miongozo ya wazi, kushika Qur'an bila stara au bila usafi kunaweza kuzoeleka na kuwa utamaduni, jambo litakalopeleka kupunguza hadhi ya Kitabu Kitukufu na kuashiria kupungua kwa uadilifu wa imani katika jamii.

Ni muhimu kukumbuka kuwa suala hili halihusu Bunge pekee; popote Qur'an inapohusishwa iwe mahakamani, kwenye sherehe rasmi, au shughuli nyingine za kitaifa, taratibu za dini lazima ziheshimiwe.

Tukio lililotokea Dodoma liwe somo. Tanzania imejengwa juu ya msingi wa kuheshimu dini zote na kuthamini mila na tunu za wananchi wake. Ili kuendeleza msingi huo, tuhakikishe vitabu vitakatifu, hususan Qur'an vinatunzwa kwa namna inayoendana na hadhi yake.

Waislamu wanawajibika binafsi kuzingatia usafi na stara wanaposhika Qur'an, na taasisi za kiserikali zinawajibika kuweka utaratibu unaolinda heshima hiyo bila kuvunja haki za mtu.

Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumelinda heshima ya dini, tumeenzi utamaduni wa kuheshimu imani za watu, na tumeimarisha taswira ya taifa letu kama nchi inayothamini maadili, ustaarabu na heshima kwa Vitabu Vitukufu.




# Katazo la vurugu na madhara yake kwa jamii

Jabir Ibn Abdillah (Allah amridhie) amesema, siku moja walitoka vitani na Mtume (rehema na amani zimshukie) pamoja na baadhi ya Muhajirina (wahamiaji kutoka Makka), mtu mmoja aliyekuwa akipenda sana utani katika wale Muhajirina akampiga mmoja wa Maanswar kwa nyuma, hivyo akapatwa na hasira mpaka watu wa pande zote mbili wakaitana.

Yule Answar akasema: "Enyi Maanswar, njooni!", na yule Muhajirina akasema: "Enyi Muhajirina, njooni!" Mtume (rehema na amani zimshukie) akatoka na kusema: "Wito huu wa kijahiliya (kijinga) ni wa nini?" Kisha akauliza: "Kumetokea nini?" Wakamueleza kuhusu kitendo cha yule Muhajirina kumpiga Answar.

Mtume akasema: "Acheni (wito wa kijahili), kwani hakika huo ni uvundo (kitu chenye harufu mbaya)!" Ndipo Abdullahi bin Ubayy bin Salul (kiongozi wa wanafiki) akasema: "Wamefikia hadi kuitana dhidi yetu? Wallahi, tukirudi Madina yule mwenye heshima zaidi atamtoa (atamfukuza) yule aliyedhalili zaidi." Umar (Allah amridhie.) akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwanini tusimuuwe huyu mtu mchafu? (akimaanisha Abdullahi bin Salul)." Mtume (rehema na amani zimshukie) akamwambia: "Hapana. Sitaki watu waseme kwamba Muhammad anaua wafuasi wake." ***[Bukhari na Muslim]***

## Mafundisho ya tukio hili:

Amani na utulivu wa mtu katika maisha yake, safari zake, makazi yake, na kuwepo mazingira rafiki yanayomuwezesha kumuabudu Mola wake bila hofu ni miongoni mwa neema kubwa za Uislamu. Allah Mtukufu anasema: "Je, hawajaona kuwa sisi tumeufanya mji huu (Makka) kuwa salama, na watu wananyakuliwa kutoka pande zote zinazowazunguka?" [Qur'an, 29:67].

## Hali za watu wengi hivi sasa

Hivi sasa umma unapitia mawimbi makubwa ya migogoro ya kisiasa na ya kijamii, huku ukiandamwa na mapinduzi yasiyo na utulivu, na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Matokeo yake ni kuenea kwa hofu, njaa, umwagaji damu na upungufu wa mali na mazao. Migogoro hii huathiri watu wengi katika itikadi zao, maadili na mitazamo yao, jambo linalosababisha kuvurugika kwa amani ya kijamii.

Usalama wa jamii umekuwa ni changamoto kubwa kwa watu na mataifa yote. Dunia inahitaji amani na utulivu ili kila mtu awe salama yeye binafsi, familia yake, na mali yake, hatimaye aweze kupata riziki yake. Mtume (rehema na amani zimfikie) amesema: "Atakayeamka miongoni mwenu akiwa na afya njema, akiwa na amani katika mji (nyumba) wake, na anamiliki chakula cha siku yake hiyo, basi atakuwa ni kama kakusanyiwa dunia (yote)." [Tirmidhi na Ibn Majah].

## Kuhamasisha fujo ni tabia ya majahili

Kama inavyoonekana katika tukio hili, utani ulikaribia kusababisha ugomvi mkubwa baina ya pande mbili za Waislamu, sauti za wito wa kuhamasisha mapigano zikasikika, lakini Mtume (rehema na amani zimshukie) akauita wito huo kuwa ni uvundo.

Amani na usalama ni miongoni mwa malengo makubwa ya dini, na ni neema kubwa kutoka kwa Allah ambayo inapaswa kushukuriwa, kulindwa na kuhifadhiwa kwa hali na mali.

Allah anasema: "Na Mwenyezi Mungu amepiga mfano wa mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikiufikia kwa nafasi kutoka kila mahali. Lakini (mji ule) ukazikufuru neema za Mwenyezi Mungu, hivyo Mwenyezi Mungu akauvika vazi la njaa na hofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyafanya." [Qur'an, 16:112].

Kwa hiyo, kutunza amani ni faradhi kutoka kwa Allah na ni msingi wa ujenzi wa jamii na ustaarabu. Allah ameunganisha kati ya neema ya riziki na neema ya amani kwa kusema: "Basi na wamwabudu Mola wa Nyumba hii (Al–Ka'aba), ambaye amewalisha kutokana na njaa, na akawapa amani kutokana na hofu." [Qur'an, 106:3–4].

Kwa sababu ya amani, jamii huishi kwa upendo, huruma, ushauri, kusaidiana, kusameheana, kuheshimiana na kushirikiana katika wema na uchamungu. Undugu wa kiimani una mchango mkubwa katika kuimarisha utulivu na kuleta amani katika jamii ya Kiislamu.

Waislamu wanapounga undugu, huchipua baina yao mapenzi, kusaidiana, kuhurumiana, kuwafanyia wema wazazi, ndugu, majirani, yatima na wajane, na huficha makosa ya wenzao badala ya kuyatangaza.

Allah anasema: "Hakika waumini ni ndugu." [Qur' an, 49:10]. Undugu uliotajwa hapa hautoi nafasi ya mtu kumdhuru ndugu yake au kuwa chanzo cha vurugu na fujo itakayosababisha ndugu zake wadhurike.

Mtume amesema: "Muislamu ni yule ambaye Waislamu wenzake wanasalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake." [Muslim]. Akasema tena: "Muumini ni yule ambaye watu wanasalimika kutokana na damu zao na mali zao." Hivyo, undugu wa kweli wa Kiislamu hujenga jamii imara yenye amani, upendo na mshikamano.

## Utii kwa viongozi na amani ya Taifa

Usalama wa jamii hauwezi kudumu bila utii kwa Mwenyezi Mungu, Mtume wake, na viongozi wenye mamlaka. Uislamu umeharamisha kuwahujumu viongozi, kueneza makosa yao hadharani, kuwahamasisha watu dhidi yao au kusababisha machafuko. Msingi wa amani ni uhusiano mzuri kati ya kiongozi na wananchi, upendo, uaminifu na ushirikiano; na hapo ndipo taifa hupata utulivu na nguvu.

جُمادى أول

MAKALA MAALUM

# Hukumu ya Kiislamu kuhusu mtu aliyetoweka

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323



Katika jamii zetu, matukio ya watu kutoweka yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara, iwe kutokana na safari ndefu, kuzama majini, kutekwa, kujiteka, migogoro, ajali, vita, au sababu nyingine zisizojulikana. Swali muhimu ambalo watu wengi huuliza ni Uislamu unasemaje kuhusu haki, mali, familia na ndoa ya mtu aliyepotea pasipo kujulikana alipo?

Makala hii inalenga kutoa mwanga, japo kidogo, kuhusu msimamo wa Fiqhi ya Kiislamu kuhusu suala hili, kwa mujibu wa maelezo ya wanazuoni mashuhuri kama yanavyopatikana katika kitabu kijulikanacho kama Fiqhu-l-Islamiy wa Adillatuhu cha Prof. Wahbah azZuḥayliy.

# Hukumu ya Kiislamu kuhusu mtu aliyetoweka

## Nani anayehesabika kama mtu aliyetoweka?

Kwa mujibu wa wanazuoni, maana ya mtu kupotea ni kutoweka au kupotea katika eneo lake, na habari zake hazijulikani kabisa, na muda ukapita kiasi kwamba haijulikani kama bado yu hai au amekufa.

Hali ya mtu aliyetoweka hutazamwa kwa misingi miwili: kwa upande wake binafsi na kwa upande wa watu wengine.

Kwa upande wake binafsi huhesabiwa kuwa hai. Hii inamaanisha kwanza, mali yake hairithiwi; pili, ndoa yake haivunjiki; na tatu anabaki kama mtu aliye hai mpaka ithibitike vinginevyo.

Kwa upande wa watu wengine huhesabiwa kama mfu. Hii ina maana kwanza, mtoweka hawezi kumrithi mtu yeyote; pili, akiachiwa wasia, hastahiki mpaka hali yake ibainike; tatu, sehemu yake katika mirathi au wasia husimamishwa hadi apatikane au hadi ithibitike wazi kama amekufa.

Madhehebu ya HanafI na Shafi yanakubaliana hasa kuhusu hukumu ya ndoa ya mke wa mtu aliyetoweka, kwamba, mke hatalazimika kukimbilia kuomba kuvunja ndoa, bali atasubiri hadi itakapothibitika kuwa mumewe amekufa.

Hata hivyo, madhehebu ya Malik na Hanbal yanatoa nafuu zaidi. Kadhi anaweza kumruhusu mke kuachwa baada ya miaka minne ya kutoweka kwa mumewe, kisha atahesabiwa kuwa katika eda ya kifo, na anaweza kuolewa tena.

## Mamlaka ya Kadhi kuhusu mali ya mtu aliyetoweka

Sheria ya Kiislamu inamlinda mtu aliyetoweka pamoja na watu wake. Kadhi ana wajibu mkubwa katika kipindi cha kutoweka kwake, kama ifuatavyo:

Mosi, kuteua msimamizi wa mali

Kadhi humteua mtu mwaminifu kutunza, kuendeleza, na kusimamia mali ya mtu aliyetoweka kama mlezi na muangalizi wa mali ya mtoto au mgonjwa wa akili.

Pili, kuuza mali inayoharibika

Ikiwa mtu aliyetoweka aliacha mali inayoharibika (kama vyakula, bidhaa zinazooza, au mali isiyodumu), kadhi atauza ili kuilinda thamani yake. Kuhusu ile mali aliyoiacha kama amana kwa watu, inaachwa mikononi mwa waliokabidhiwa ili kuihifadhi.

Tatu, kutunza familia yake kwa mali yake

Kadhi hutumia mali ya mtu aliyetoweka kuwalisha na kuwahudumia wafuatao. Kwanza, mke wake, endapo ndoa bado ipo; pili, watoto wake wadogo; na tatu watoto wake maskini au tegemezi na wasioweza kujitunza.

Kama mali yake inapatikana katika fedha, chakula, au nguo; matumizi hutolewa moja kwa moja. Lakini kama mali yake ni majengo au bidhaa za biashara, kadhi hapaswi kutoa matumizi kwa kuuza mali hizo, kwa kuwa hana ruhusa ya kuzibadilisha bila sababu maalum.

Ni baba pekee wa aliyepotea ndiye anaweza kuuza bidhaa za mtoto wake kwa sababu ana mamlaka ya malezi ya kifedha; lakini linapokuja sual la kuuza majengo kunahitaji ruhusa ya kadhi.

## Ni lini Kadhi atatangaza mtu aliyetoweka amefariki?

Kadhi hatoi hukumu ya kifo kwa kukurupuka au haraka. Badala yake, sheria inasema kwamba ukishapita muda mrefu kiasi ambacho watu wa rika lake hawawezi kuishi mpaka kufikia kipindi au muda huo, kadhi atamhukumu kuwa amekufa.

Athari za hukumu hii ni kwanza, ndoa yake inavunjika; pili, mali yake inagawanywa kwa warithi wake walio hai; na tatu, yeye hashiriki tena katika mirathi ya yeyote mwingine.

## Je, muda wa mwisho ni miaka mingapi?

Katika riwaya mashuhuri ya maimamu wa Hanafi, hakuna muda maalum, bali huzingatiwa umri wa kuishi wa watu wa kizazi au rika lake.

Hata hivyo, imepokewa kutoka kwa Imam Abu Hanifa kuwa muda huo ni miaka 120 tangu kuzaliwa lakini baadhi ya wanazuoni wameeleza kuwa miaka 90 ndiyo inayofaa zaidi kutokana na urahisi wa mambo.

Ama kwa madhehebu ya Malik na Hanbal, muda wa kutengua ndoa si ule wa kutangaza kifo bali ni miaka 4 tu, endapo mume hatapatikana.

## Mwisho

Kwa kweli Sheria ya Kiislamu imetengeneza mfumo ambao kwa busara unalinda haki za mtu aliyetoweka, usalama wa familia yake, usalama wa mali yake isiendelee kupotea, haki za warithi wake, na muhimu zaidi tulivu wa jamii. Kwa mazingira yetu ambako watu kutoweka kunazidi kuwa jambo linalohitaji mwongozo wa kisheria na kidini, ni matarajio yangu mafundisho haya yatatoa dira muhimu kwa ustawi wa jamii, mitandao ya haki za binadamu, mahakama za mambo ya kifamilia, viongozi wa dini, na wanajamii wanaotaka kufanya maamuzi ya haki na yenye huruma kwenye uga huu.


Afya
Pure Drinking water

"Afya" is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.




WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com

جمادى أول

# فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

***Swali:*** **Nimepotelewa na mpwa wangu kwenye vurugu za tarehe 29/Oktoba/2025, Je, Uislamu unamzungumziaje kuhusu mtu asiyejulikana alipo na tusiyejua kama yu hai au amekufa?**

***Jawabu:*** Katika fiqhi ya Kiislamu, suala la "al-Mafqud" (mtu aliyepotea au asiyejulikana kama yu hai au amekufa) limejadiliwa kwa upana na wanazuoni.

Kifupi hakuna muda mmoja uliokubaliwa na madhehebu yote; hukumu ya mkasa huo hutegemea qiyas (ulinganishaji), maslaha, na utaalamu wa wanazuoni kulingana na hali ya kijamii na mazingira yaliyotokea. Ufuatao ni muhtasari na mtazamo wa madhehebu mbalimbali:

## 1. Madhehebu ya Hanafi

■ Hawakuweka muda maalum wa kudumu kwa mtu aliyetoweka (mafqud).

■ Mtu aliyepotea hachukuliwi kuwa amekufa mpaka kuwe na dalili madhubuti za kifo, kama vile kupatikana habari za kuaminika.

■ Kama hakuna dalili, hukumu yake ni kama yupo hai; mali yake haigawiwi, ndoa yake haivunjwi, nk.

■ Baadhi ya wanazuoni waliruhusu kadhi kuweka muda fulani kwa mujibu wa kiasi cha muda mtu kama huyo anaweza kuishi kawaida kwa makadirio ya watu wa umri wake.

## 2. Madhehebu ya Malik

■ Wameweka ukomo maalumu katika mazingira ya kawaida: Mafqud anasubiriwa hadi kufikia umri ambao kawaida watu huonekana hawaishi tena.

■ Mara nyingi wanataja umri huu kuwa 60, 70 – 80 au kufikia umri wa kufariki wa wenziwe Imepokewa hadithi na Swahaba Abu Huraira (Allah amridhie) akieleza kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisema: "(Wastani wa) umri wa kuishi umati wangu ni kati ya miaka sitini na sabini ni wachache mno wanaovuka hapo" Rejea Tirmidhi, Ibn Majah na wengineo

■ Wakati huo ukifika, anaweza kuhukumiwa kuwa amekufa bila kutegemea dalili nyingine.

## 3. Madhehebu ya Shafi

■ Kauli mashuhuri; yenye nguvu ni kuwa hakuna muda maalum; bado huchukuliwa kuwa hai mpaka ithibiti kinyume chake.

■ Lakini baadhi ya Shafi waliruhusu kadhi aamue muda kwa kulihusisha suala hilo na kwanza, mazingira ya kupotea; pili, uwezekano wa kuendelea kuishi; na tatu ushahidi wa kijamii.

4. Madhehebu ya Hanbali

■ Wanayazingatia mazingira ya kupotea.

■ Mosi, iwapo alipotea katika hali ya hatari (vita, janga, safari ya bahari) baadhi ya riwaya zinasema asubiriwe hadi miaka nne, kisha anaweza kuhesabiwa kuwa amekufa.

■ Kwa upande mwingine, akipotea katika mazingira salama, basi husubiriwa hadi umri ambao kawaida watu hawaishi zaidi, mfano 70–80.

5. Mtazamo wa wanazuoni wa karne za hivi karibuni

Sababu za kisasa kama uwezo wa kutafuta watu kupitia teknolojia mbalimbali, ikiwemo picha za satelaiti, simu za mkononi na kadhalika; uchunguzi wa DNA; taarifa za serikali; na hali za vita au majanga zimesababisha kadhi au mahakama za Kiislamu kuruhusiwa kuamua muda wa kumsubiri mafqud kulingana na mazingira ya nchi.

Katika nchi nyingi za Kiislamu leo, miaka 4 hutumika kwa aliyepotea katika hali za hatari (mfano: vita), na miaka 7–10 hutumika kwa mazingira yasiyo hatari, ingawa si sheria ya Kiislamu ya lazima bali ni ijtihadi ya mahakama.

## Kwa Muhtasari

Hakuna muda mmoja wa Kiislamu uliowekwa kwa wote.

■ Muda hutegemea madhehebu, aina ya kupotea, na maamuzi ya kadhi.

■ Kwa madhehebu ya Hanafi na Shafi haisemwi muda maalum bali anachukuliwa kuwa yu hai hadi ithibitike amekufa.

■ Kwa upande wa Malik na baadhi ya Hanbali, muda unahusishwa na umri wa kawaida wa kuishi ( miaka 70 – 80).

■ Riwaya nyingine za Hanbal, ikiwa kupotea kulikuwa katika mazingira ya hatari — muda wa kusbubiri ni miaka 4.

جُمادى أول

HABARI KIMATAIFA

MAHMOUD NYAMGUMA

# Azimio la Baraza la Usalama kuhalalisha ukaliaji wa Gaza?



Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linatarajiwa kupiga kura kuhusu azimio jipya linalounga mkono mpango wa amani wa Rais wa Marekani, Donald Trump, kuhusu mgogoro wa Gaza.

Azimio hili limeibua mjadala mpana duniani, si tu kuhusu mustakabali wa vita ya miaka miwili kati ya Israel na Hamas, bali pia kuhusu maisha ya watu wa Gaza na historia pana ya ukiukwaji wa haki za Wapalestina.

Mpango huu unapendekeza kuundwa kwa "Board of Peace", chombo cha muda kitakachokuwa na mamlaka ya kuongoza Gaza hadi 2027—ikiwa ni hatua inayompa Marekani, na hasa Trump, nafasi ya kipekee katika masuala ya ndani ya Palestina.

Pia unapendekeza kuundwa kwa International Stabilization Force (ISF) itakayoshirikiana na Israel, Misri, na polisi wa Kipalestina waliopatiwa mafunzo mapya katika kuhakikisha usalama na "kuondoa silaha" ndani ya Gaza.

## Lakini nini maana ya kura hii kwa watu wa Gaza?

Kwa zaidi ya miaka saba, Gaza imekuwa ni eneo lililokumbwa na maumivu yasiyoelezeka, vifo vya raia, uharibifu wa miundombinu, kufungwa kwa mipaka, na ukosefu wa huduma za msingi.

Wapalestina wengi wamekuwa wakitamani kuona mwisho wa vita na mwanzo mpya. Hata hivyo, swali linalobaki ni: je, azimio hili ni suluhisho au mwendelezo wa mateso yao?

Kwanza, ISF inayopendekezwa, ikiwa ipo chini ya ushawishi wa Marekani, Israel, na Misri, inaibua wasiwasi mkubwa kwamba inaweza kuwa chombo cha kuhalalisha udhibiti wa kimataifa badala ya kuleta amani ya kweli.

Wapalestina wamewahi kushuhudia mara kadhaa maamuzi ya kimataifa yanayowekwa juu yao bila ushirikishwaji wa kina wa uongozi wao halisi. Pia, maswali yanabaki kuhusu jukumu la Mamlaka ya Palestina na uhalali wa Trump "kuongoza" Gaza kwa njia yoyote ile.

## Je, kura hii inaweza kuwa hatua ya kihistoria kufuta dosari za zamani?

Kwa miongo mingi, historia ya mgogoro wa Palestina na Israel imejengwa juu ya matukio ya ukiukwaji wa haki, ukandamizaji, na unyakuzi wa ardhi. Wakosoaji wanasema kuwa haijalishi ni maneno gani mazuri yanawekwa kwenye azimio, ukweli unabaki kuwa: hakuna amani ya kudumu bila uwajibikaji wa Israel kwa ukiukwaji wa haki za binadamu uliofanyika Gaza na maeneo mengine.

Rasimu ya Urusi inaonekana kutambua hili kwa kusisitiza juu ya suluhisho la mataifa mawili na kupinga kuanzishwa kwa vyombo vipya vya utawala vinavyopendekezwa na Marekani. Swali linabaki: kwa nini rasimu ya Marekani haikujumuisha wazi msingi wa suluhisho hilo? Ni kwa maslahi ya nani?

Je, mkakati huu unaolenga "utulivu" unaweza kuandaa mazingira ya haki, uwajibikaji, na uhuru, au ni jaribio la kusukuma mbele ajenda za kisiasa za mataifa yenye nguvu?

## Hofu ya kurejea katika mzunguko ule ule

Balozi wa Marekani, Mike Waltz, anasema kuwa kupinga azimio la Marekani ni "kumpa Hamas mamlaka" au "kurudi vitani." Lakini hoja hii inasahaulisha ukweli kwamba wengi wa waliouawa ni raia wasiokuwa na hatia, na kwamba maamuzi ya Baraza la Usalama mara nyingi yameshindwa kuwalinda Wapalestina.

Ikiwa azimio hili litaidhinishwa bila marekebisho muhimu, kuna hatari kwamba Gaza itakuwa eneo linalodhibitiwa kimataifa bila uhuru wa kisiasa, huku historia ya ukandamizaji ikisahaulika kwa jina la "utulivu."

Gaza haihitaji mpango unaojenga utulivu kwa faida ya mataifa makubwa; inahitaji amani yenye haki, uhuru wa kweli, na utawala unaosimamia maslahi ya wananchi wake.

# Ziara ya Waziri Afrika Kusini aliyeishtaki Israel yazua mjadala Marekani

Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini, Naledi Pandor, ambaye aliongoza kesi ya kuipeleka Israel katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) kwa tuhuma za mauaji ya kimbari dhidi ya Wapalestina, anatarajiwa kuwasili Marekani Alhamisi, katika ziara ambayo imezua mjadala mkali miongoni mwa wanaharakati wa Kiislamu, wanadiplomasia na wataalamu wa sheria za kimataifa.

Safari yake inakuja wakati ripoti mbalimbali, ikiwemo ile ya UN OCHA, zinaonesha kuwa zaidi ya Wapalestina 38,000 wameuawa Gaza tangu Oktoba 2023, idadi ambayo imekuzwa kama ushahidi wa kile kinachoonekana kuwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Pandor, ambaye ni Muislamu aliyebadili dini miaka kadhaa iliyopita, amekuwa sauti muhimu katika bara la Afrika kuhusu utetezi wa haki za Wapalestina. Alikaririwa akisema kuwa "Waislamu ni watu wa amani, lakini wanaruhusiwa kujitetea pale haki inapokanyagwa," akisisitiza misingi ya kimataifa inayotambua resistance ya watu wanaokabiliwa na ukaliaji wa mabavu.

Kauli zake zimeungwa mkono na makundi kadhaa ya Kiislamu barani Afrika na Mashariki ya Kati, huku wachambuzi wa siasa wakibainisha kuwa msimamo wake unatoa changamoto kwa msimamo wa nchi nyingi za Magharibi zinazotuhumiwa kupuuza mauaji ya raia Gaza.

Hata hivyo, vyombo vya habari vya Marekani vinadai kuwa mawasiliano yake ya simu na Ismail Haniyeh siku chache baada ya mashambulizi ya Oktoba 7, 2023, yameibua shinikizo kwa serikali ya Marekani kutathmini upya kibali chake cha kuingia nchini humo.

Wakati ofisi yake ilisisitiza kuwa mazungumzo yalihusu misaada ya kibinadamu, vyanzo vya serikali ya Marekani vimeeleza kuwa wanapitia "utaifa na misimamo ya Pandor baada ya kuiongoza Afrika Kusini katika kesi ya kisheria dhidi ya Israel."

Ziara yake inatarajiwa kukutana na malalamiko kutoka makundi ya kihafidhina ya Marekani, ingawa kwa upande mwingine, Waislamu wa Marekani, wanaharakati wa haki za binadamu, na mashirika ya Kiislamu kama Muslim Network TV na Sound Vision, wanamwona Pandor kama "mwanamke jasiri aliyesimama wakati viongozi wengi wa Kiislamu waliponyamaza."


Katika waraka wa maandalizi ya hafla yake Milwaukee, waandaaji wanamsifu kwa "kukabiliana na ukimya wa ulimwengu kuhusu mauaji ya Gaza," wakimrejea kama nembo ya ujasiri wa kidiplomasia wa Afrika. Huku akisubiri uamuzi wa mwisho wa Idara ya Jimbo la Marekani, wachambuzi wa siasa za Mashariki ya Kati wanasema kuwa Pandor anabeba "mfano wa Afrika mpya", Afrika inayokataa historia ya ukoloni na inayodai uwajibikaji wa kimataifa dhidi ya mauaji ya raia.

## Wabunge Uingereza: Serikali itambue tatizo la Islamofobia

**Kundi la wabunge 40 wa Chama cha Labour na wabunge huru limeitaka serikali ya Uingereza kuidhinisha rasmi tafsiri ya Islamophobia, baada ya takwimu kuonyesha makosa ya chuki dhidi ya Waislamu yameongezeka karibu asilimia 19 katika mwaka uliopita.**

**Barua hiyo, iliyoandikwa na Mbunge Afzal Khan na kutumwa kwa Waziri wa Makazi, Jamii na Serikali za Mitaa, Steve Reed, imetiwa saini na wabunge miongoni mwao Diane Abbott, Dawn Butler, Kim Johnson na Andrew Gwynne, ikieleza kuwa mwaka 2025 takribani asilimia 45 ya makosa ya chuki za kidini yaliwalenga Waislamu.**

**Barua hiyo iliyonukuliwa na gazeti la Guardian la Uingereza, imesisitiza kuwa makosa ya chuki dhidi ya Uislamu yamepanda jumla ya asilimia 92 tangu 2023, hivyo serikali ichukue "hatua muhimu" ya kuweka ufafanuzi wa chuki dhidi ya Waislamu.**




**Serikali ilianzisha Februari mwaka huu kikosi kazi cha kuandaa maelezo ya kile kinachotafsiriwa kama matendo yasiyokubalika, ubaguzi, chuki na mashambulizi dhidi ya Waislamu au wanaodhaniwa kuwa Waislamu. Taarifa inaeleza kuwa kikosi kazi hicho, kinachoongozwa na wakili Dominic Grieve KC na kuhusisha wataalamu wakiwemo Akeela Ahmed na baronesi Shaista Gohir, tayari kimekabidhi ripoti yake kwa waziri na serikali "inaichunguza". Wabunge hao wanataka tafsiri hiyo iidhinishwe wakati wa mwezi wa uhamasishaji dhidi ya Islamophobia mwezi Novemba na kwa ushirikiano na jumuiya za Kiislamu ambazo zinapaswa kulindwa. Serikali za zamani za Conservative zilikuwa na wasiwasi kuwa tafsiri za awali zingezua hofu ya kufifisha uhuru wa kujieleza, lakini ripoti za awali zimeeleza kuwa pendekezo jipya litahifadhi haki ya kuikosoa dini.**

**Msemaji wa Wizara ya Makazi na Jamii amesema idara "inaangalia kwa makini mapendekezo ya kikosi kazi na itajibu wakati muafaka."**

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
+255 789 201383

# Serikali ipongezwe ujenzi shule za elimu ya amali

Tumefurahishwa na habari kwamba wanafunzi 2,267 wa kidato cha pili wamefanya Mtihani wa Upimaji wa masomo ya amali kwa mara ya kwanza mwaka huu, kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (toleo la 2023) na Mtaala ulioboreshwa.

Hii ni hatua ya kupongezwa, kwani inalenga kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi wa ufundi na ujasiriamali ili kumudu maisha yao, kushindana katika soko la ajira na kuchangia maendeleo ya Taifa.

Tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujenga shule mpya 103 za sekondari za amali ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kati ya shule hizo, 29 ni za amali za kihandisi na shule 74 ni za amali zisizo za kihandisi.

Kujengwa kwa shule hizo ni hatua muhimu kwa nchi, hasa ikizingatiwa kuwa elimu yetu imekuwa ikilalamikiwa kwa kuandaa wahitimu wasio na stadi za kazi, hali inayosababisha tatizo la ajira kuwa kubwa.

Kwa lugha ya kidini, Rais Samia ametekeleza matakwa ya Uislamu na wajibu wake kama kiongozi mkuu wa nchi. Katika hadith iliyonukuliwa na Muslim, Mtume Muhammad (rehema za Mwenyezi Mungu na amani iwe juu yake) amesema: "Na anayefuata njia kwa ajili ya kutafuta elimu, Mwenyezi Mungu humsahilishia yeye njia ya kuelekea Peponi." [Muslim].

Kisha Mtume akaonya: "Atakayeulizwa kuhusu jambo (elimu) nae akaificha, Siku ya Kiyama atachomwa na chuma cha moto." [Abu Daudi na Tirmidhi]. Kwa hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wamiliki wa shule na vyuo binafsi wana wajibu wa kuhakikisha mitaala iliyopo inatumika kuandaa rasilimali watu yenye ujuzi na maarifa stahiki kwa maendeleo ya Taifa.

Sambamba na jitihada za kuongeza shule za sekondari za amali nchini, vilevile ni muhimu kuendelea kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi, lakini pia kuwajengea uwezo wakufunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Kwa kuzingatia kuwa lengo kuu la elimu ya amali ni kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa kutenda, ni vyema wadau mbalimbali wa sekta ya elimu kutumia muda uliobaki kutoa mapendekezo yao kuhusu Sheria ya Elimu ambayo inafanyiwa mapitio.

Hata hivyo, ili kufikia malengo kusudiwa ni lazima kuwepo kwa vitendea kazi vya kutosha katika shule ili kuwezesha utekelezwaji wa mafunzo ya ufundi, na pia kuandaa walimu wa kufundisha masomo ya amali ili kukidhi mahitaji katika shule za msingi na sekondari.

Ni jambo la kutia moyo kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeanzisha mitaala mipya sita ya kufundisha walimu wa masomo ya amali ili kupata walimu stadi watakaoendana na mabadiliko ya mfumo wa sasa wa elimu.

Mitaala hiyo ambayo itaanza kutumika mwaka huu wa masomo ni Shahada ya Ufundishaji wa Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo, Shahada ya Ufundishaji wa Ushonaji na Mitindo ya Mavazi, na Shahada ya Ufundishaji wa Bustani na Mboga.

Shahada nyingine ni ya Ufundishaji wa Lishe na Huduma ya Chakula, Shahada ya Ufundishaji wa Ufugaji wa Viumbe wa Majini, na Shahada ya Ufundishaji wa Uzalishaji wa Mifugo.

Kimsingi, kozi hizi zote zinalenga kujenga uwezo wa walimu kufundisha stadi za maisha shuleni na kuandaa kizazi cha vijana wabunifu na wachapakazi watakaoweza kujiajiri na kuajiriwa.

Tunarudia kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kujenga shule mpya za amali 103, tukiamini kuwa ni uwekezaji bora na wenye tija katika kuandaa wanafunzi wenye uwezo wa kuchangia uchumi wa nchi.

جمادى أول

MAKALA MAALUM



NA SHEIKH SEIF RUGA

# Sababu tano za waumini kujaribiwa na Alllah

Wakati mwingine Muislamu anaweza kuwa na daraja kubwa mbele ya Allah Mtukufu, lakini hawezi kufikia daraja hiyo kwa matendo yake mema tu. Ni kwa sababu hiyo, Allah Mtukufu humjaribu mja kwa kumpa masaibu, shida au dhiki, kisha humpa uvumilivu na hatimaye kumpandisha daraja.

Mitihani na majaribu ni miongoni mwa mienendo na kanuni za Allah Mtukufu. Yeye (Allah) huwajaribu waja wake waumini kwa dhiki kama anavyowajaribu kwa neema, huwapima kwa matatizo kama anavyowapima kwa neema, huwapima kwa shari kama anavyowapima kwa kheri.

Ama wale wasiomuamini Allah na wenye mitazamo ya kikafiri hupandikiza shaka na wasiwasi katika nyoyo za Waumini kuhusu majaribio na mitihani ya Allah. Husema: "Kwanini Allah ameumba shari na mitihani hapa duniani?" Wamesahau kuwa dunia ni mahali pa mtihani, si mahali pa malipo kwani malipo ya haki yapo Akhera na wala si duniani.

Pia wanahoji: "Ikiwa Allah Mtukufu anawapenda waja wake kwanini basi awape mitihani na masaibu mengi?" Jibu ni kwamba, wapingaji hawa wanashindwa kutofautisha kati ya mitihani ya Allah kwa waja wake wapendwa (ili kuwainua kidaraja), na adhabu ya Allah kwa maadui zake (ili kuwaonya au kuwaangamiza). Muislamu wa kweli anafahamu tofauti hii.

Mja anapotambua siri na hekima ya Allah katika kuleta mitihani hupokea masaibu hayo kwa moyo mkunjufu bila ya kinyongo, huwa mtulivu kwa yakini ya hekima ya Mola wake, hukubali maamuzi ya Allah Mtukufu kwa kuridhia kadari yake, na katika hali hiyo hujikurubisha zaidi kwa Mola wake Mlezi.

## Hekima ya waja kupewa mitihani

Mosi, kumlilia Allah na kujinyenyekeza kwake

Allah Mtukufu anapenda kumuona mja wake akimlilia kwa unyenyekevu na dua wakati wa dhiki na matatizo – na hii ni njia ya mja kurejea kwa Mola wake. Allah anasema: "Na kwa yakini tulipeleka Mitume kwa kaumu zilizokuwa kabla yako, kisha tukazitia katika dhiki na mashaka ili zipate kunyenyekea..." [Qur'an, 6:42].

Katika kuifasiri aya hii, Imam Ibn Kathir amesema, dhiki maana yake ni umasikini na ugumu wa maisha; na mashaka ni magonjwa, mateso na maumivu yanayowapata waja ili wainamishe vichwa vyao na kumuomba Allah kwa unyenyekevu,

Ni jambo zuri na lenye baraka kwa Muislamu kukabiliana na shida kwa kumlilia Mola wake, badala ya kuipokea kwa hasira, lawama au malalamiko. Kupata masaibu huwa ni njia ya kurejea kwa Allah, na si sababu ya kupotoka.

## Pili, kuharakishiwa adhabu ya duniani

Wakati mwingine Allah humharakishia mja wake adhabu ya duniani Ili arejee kwake kwa toba na msamaha, kwani adhabu ya Akhera ni kali zaidi na ni kubwa mno. Hivyo basi, iwapo mja ataadhibiwa hapa duniani kabla ya Akhera, hilo litakuwa ni kheri kwake, kwa sababu kupitia adhabu hiyo atafika kwa Mola wake akiwa tayari ametakasika na madhambi kutokana na adhabu alizopata hapa duniani.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Allah anapotaka kumtendea wema mja wake humharakishia adhabu yake hapa duniani; na anapotaka kumtendea shari mja wake humcheleweshea adhabu hiyo hadi amkute nayo Siku ya Kiyama."

## Tatu, kufutiwa madhambi

Muislamu anayejitahidi kutafuta radhi za Mola wake huumizwa na madhambi aliyofanya, hivyo hujitahidi kutafuta njia za kuyafuta. Miongoni mwa njia kubwa za kufuta madhambi ni kupitia mitihani na masaibu. Mtume amesema: "Muislamu hapati uchovu, wala maradhi, wala huzuni, wala maumivu, wala dhiki, wala shida, hata kuchomwa na mwiba isipokuwa Allah humfutia baadhi ya madhambi yake kwa hilo." [Bukhari na Muslim].

## Nne, kunyanyuliwa daraja

Wakati mwingine muumini anaweza kuwa na daraja tukufu mbele ya Allah Ta'ala ambayo hawezi kuifikia kwa matendo yake ya kawaida. Hapo ndipo hekima ya Allah huingia kwa kumpa mtihani na kisha kumpa uwezo wa kustahimili kwa subira. Kwa njia hiyo, mja hufikia daraja aliyokusudiwa.

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Hakika malipo makubwa kabisa yapo pamoja na mtihani mkubwa, na hakika Allah anapowapenda watu huwapa mitihani. Basi atakayeridhia (mtihani huo) atapata radhi za Allah; na atakayekasirika atapata ghadhabu (za Allah)." [Tirmidhi]. Muumini hawezi kuimarika na kustahiki daraja kubwa hadi apitie mtihani kisha avumilie.

Imam Shafi (Allah amrehemu) alipoulizwa ni lipi bora zaidi kati ya mtu kupewa utukufu au kujaribiwa alijibu: "Hatapewa utukufu hadi ajaribiwe." Kisha akataja kuwa, Mitume waliopata hadhi ya juu – yaani Mtume Nuh, Ibrahim, Musa, Isa, na Mtume Muhammad (amani iwe juu yao) – wote walipitia mitihani mikubwa kabla ya kufikia daraja zao.

## Tano, kupimwa imani

Allah anatuambia: "Huenda mkachukia kitu na ndani yake kuna kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu na ndani yake kuna shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui." [Qur'an, 2:216].

Nae Mtume (rehema za Allah na amani ziwe juu yake) amesema: "Ajabu ya hali ya muumini! Kila jambo lake ni kheri; anapopatwa na furaha hushukuru na huwa kheri kwake, na anapofikwa na madhila huvumilia na huwa kheri kwake, na haiwi hivyo (sifa hiyo) ila kwa Muumini." [Muslim].

جمادى أول

NASAHA ZA WIKI



NA YUSUFU AMINI
0787 503 085

# Hakuna aliyefilisika kwa kutoa zaka

Tumeelezwa katika Qur'an kuwa, sisi wanadamu ni wasimamizi tu katika vile alivyotupa Allah, na hatuna umiliki wa hakika bali mmiliki wa vyote ni Yeye peke yake. Allah ameagiza tutoe katika vile alivyotupa dhamana ya usimamizi kwa kusema: "...na toeni katika vile alivyokufanyeni nyinyi (Mwenyezi Mungu) kuwa ni waangalizi wake. Basi walioamini miongoni mwenu, na wakatoa, wana malipo makubwa." [Qur'an, 57:7].

Utoaji huu ni pamoja na zaka kwa ajili ya kutaka radhi za Allah Ta'ala. Kiujumla, kutoa zaka ni katika ibada muhimu zilizohimizwa katika dini yetu tukufu ya Uislamu. Aidha, utoaji zaka umehimizwa kwa sababu humkinga mtu na mabalaa mbalimbali ya kimaisha, lakini pia humuweka karibu na Muumba wake.

Kutokana na utukufu wa nguzo ya zaka, Allah 'Azza Wajallah' aliipa umuhimu nguzo hii kwa kuifaradhisha katika mwaka wa pili wa Hijriyya na baadae akabainisha viwango vyake na aina ya watu wanaosatahiki kupewa zaka.

Katika kuifasiri aya: "Na ambao wanatoa zaka." [Qur'an, 23:4], Imam Ibn Kathir amesema: "Wanazuoni wengi wanasema kuwa zaka (iliyokusudiwa katika aya hii) ni ya mali, licha ya kuwa aya imeshuka Makka. Kinachodhihiri ni kwamba, zaka iliwajibishwa katika mji wa Makka na kilicholetwa Madina ni ubainifu wa viwango vyake tu kama inavyosema aya nyingine iliyoshuka Makka: "...na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake." [Qur'an, 6:141].

Pamoja na ubainifu huo, bado Waislamu wengi hawaoni umuhimu wa kutoa zaka. Matokeo yake, watu wengi ndani ya jamii zetu wanaishi katika lindi la umasikini, huku kula yao ikiwa ya kubahatisha, wanakosa mavazi ya uhakika, nyumba zenye hadhi, na mahitaji mengine muhimu.

Kwa upande mwingine, wapo watu wachache katika jamii yetu wanaoogelea katika maisha ya raha, na hawaoni haja ya kuwasaidia masikini. Ifahamike wazi kuwa, kutoa zaka siyo hisani bali ni wajibu unaomhusu kila Muislamu aliyefikia kiwango cha kutoa zaka (Nisab).

Hata hivyo inastaajabisha kuona Waislamu wengi wameghafilika na kutekeleza jambo hili adhimu katika Uislamu. Zaka siyo tu inaweza kutokomeza umasikini, bali pia ni njia ya kuwaleta pamoja Waislamu na watu wa imani nyingine. Katika ibada ya utoaji zaka, Allah anawatoa hofu waja wake na kuwathibitishia kuwa, wanapotoa huibariki mali yao na kuizidisha maradufu.

Anasema: "...na mkopesheni Mwenyezi Mungu mkopo mwema. Na kheri yoyote mnayoitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaikuta kwa Mwenyezi Mungu imekuwa bora zaidi, na ina thawabu kubwa sana..." [Qur'an, 73:20]. Pia, Allah amesema katika Hadithil Qudsy: "Ewe mwanadamu! Toa nami nitakuzidishia." [Bukhari na Muslim].

Hivyo basi, njia bora ya kuchuma ziada ya kile ulichonacho ni kutoa zaka ili Allah aendelee kukufanyia wepesi katika njia za chumo lako. Na wala huwezi kufilisika kwa sababu ya kutoa zaka. "Sema, 'Kwa hakika Mola wangu Mlezi humkunjulia riziki na humdhikisha amtakaye katika waja wake. Na chochote mtakachokitoa Yeye atakilipa. Naye ni Mbora wa wanaoruzuku.'" [Qur'an, 34:39]. Zipo faida nyingi kwa mwenye kutekeleza ibada ya zaka.

Kwanza, zaka ni ibada inayoleta manufaa endelevu katika jamii, kwa sababu mwenye mali anamuhurumia mnyonge na kumfanyia hisani, kama ambavyo Allah amemfanyia yeye hisani. Mwenyezi Mungu anasema: "Nawe fanya wema kama Allah alivyokufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Allah hawapendi mafisadi." [Qur'an, 28:77].

Pili, zaka ni ibada inayokamilisha Uislamu wa mtu. Mwenye kutoa zaka anakuwa ameikamilisha dini yake, jambo litakalomletea furaha katika maisha yake ya hapa duniani na kesho Akhera.

Tatu, kutoa zaka humfanya mtu kuwa mtiifu kwa Allah Aliyetukuka na kutekeleza amri zake. Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) amesema: "Nimeamrishwa (na Allah) kupigana dhidi ya watu hadi waape kwamba, 'Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni mjumbe wake', na kusimamisha sala na kutoa zaka. Hivyo, wakiyatekeleza hayo sitawasumbua kwenye maisha yao na mali zao isipokuwa kwa sharia za Kiislamu, na hesabu yao itafanywa na Allah.'" [Bukhari na Muslim].

Nne, zaka hujenga uhusiano mzuri kati ya matajiri na masikini, lakini pia huondosha chuki, hasira na husuda katika nyoyo za watu masikini kutokana na kupewa fungu la zaka katika mali za matajiri.

Tano, zaka inasaidia kuzitakasa nafsi na kuzikinga dhidi ya maradhi ya choyo na ubahili. Mwenyezi Mungu anasema: "Chukua sadaka (zaka) katika mali zao, uwasafishe na kuwatakasa kwa ajili ya hizo (mali zao)." [Qur'an, 9:103].

Sita, zaka humjengea mtu tabia ya ukarimu, kuwahurumia wahitaji na kuwafanyia upole mafukara.

Saba, kutoa zaka ni sababu ya kuingia Peponi, kama ilivyothibiti katika hadith iliyopokewa na Malik Al–Ash'ar (Allah amridhie) aliyesimulia kuwa, Mtume (rehema za Allah na amani imshukie) amesema: "Hakika katika Pepo kuna chumba ambacho nje yake kinaonekana kama ndani, na ndani yake kinaonekana kama nje. Allah Aliyetukuka amemuandalia (chumba hicho) mwenye kulisha masikini, mwenye kuzungumza lugha ya staha, mwenye kufunga swaumu, mwenye kusalimia watu kwa wingi, na mwenye kusali usiku wa manane hali ya kuwa watu wamelala." [Tirmidhi].

Nane, zaka huzuia vitendo vya uhalifu kama wizi, uporaji, ujambazi wa kutumia silaha, udokozi, na ukahaba. Iwapo matajiri watatoa zaka ipasavyo, hapana shaka vitendo hivi viovu vitapungua kama si kuisha kabisa. Na kama watatoa zaka kikamilifu, basi chuki na hasira dhidi ya matajiri zitaondoka.

جمادى أول

SEHEMU YA
4

MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494



# ZAINAB BINT JAHSH
## Mke wa Mtume

# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**SWAHABA tunayemzungumza leo ni mmoja ya wake za Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie). Yeye aliitwa Zainab bint Jahsh bin Riyab, bin Ya'mar bin Swabra bin Murra bin Kathir bin Ghunmi bin Daud bin Asad bin Khuzaima (Allah amridhie). Zainab alizaliwa Makka na mama yake ni Umayma bint Abdil Mutwalib bin Hashim bin Abdi Manaf.**

### Mahusiano yake na Mtume

Zainab, licha ya kwamba ni mtoto wa shangazi wa Mtume, pia alikuwa ni mmoja wa wake zake mashuhuri hivyo ni Mama wa Waislamu.

Huyu ni katika Maswahaba wanawake waliosilimu mapema kabisa na alisifikana kwa uzuri wa sura na umbo, uchamungu kushika dini, ukarimu na pia kama miongoni mwa wanawake waliojivunia heshima kubwa katika familia na jamii yake.

### Kuolewa kwake na Mtume

Zainabu kabla ya kuolewa na Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) aliolewa na Zaidu bin Haritha lakini ndoa yao ilikumbwa na migogoro, na Zaidu akamuacha. Alipoachwa, ndio akaolewa na Mtume kwa amri ya Allah.

Zainab aliolewa akiwa na umri wa miaka 25 katika mwezi wa mfungo pili mwaka wa tano Hijiriya, akifuata baada ya Ummu Salama kuolewa, kama anavyoelezea mwanazuoni bobezi wa historia Ibn Is-hak. [Taz. Rijal wa nisaa hawla rasoul uk 114].

### Kisa cha kumuoa

Ndoa ya Mtume kwa Zainab ilitofautiana na ndoa zake kwa wanawake wengine kama tulivyogusia hapo juu. Tumeeleza kwamba, Zainab, kabla ya aliolewa na Zaidu bin Haritha, ambaye huyu alikuwa mtumwa ambaye Mtume alipewa zawadi na kisha akamuacha huru na kumlea kama mwanawe.

Ndoa ya wawili hao haikudumu lakini wakati huohuo katika jamii ya Waarabu ya wakati huo, ilikuwa ni uchuro mtu kumuoa mwanamke aliyekuwa mke wa mtoto wake wa kupanga (si wa kumzaa).

Sharia ya Kiislamu ilitaka kuondoa ada hii isiyo na mantiki yoyote na kuwaondolea uzito Waislamu wa kuwaoa wanawake kama hao pindi wanapoachika kwa watoto wao wa kupanga (kuwale); na Allah alishahukumu Mtume awe wa kwanza kuitekeleza sharia hiyo.

Katika sura ya 33 aya ya 40, Qur'an inasema: "Muhamad si baba wa yoyote katika vijana wenu, lakini yeye ni Mtume wa Allah na mwisho wa Mitume, na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu."

Hapa, katika hatua ya kwenda kuharamisha desturi iliyozoeleka, Qur'an ilitanabahisha kwamba Zaidu si mtoto wa Mtume kama walivyokuwa wakimuita Zaidu bin Muhammad.

Ikumbukwe kuwa wakati aya hii inashuka, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) hakuwa na mtoto wa kiume. Vijana wake wote walishafariki zamani. Qur'an ikaelekeza: "Waiteni kwa (ubini) wa baba zao, huo ndio uadilifu mbele ya Mwenyezi Mungu, na kama hamuwajui baba zao, basi ni ndugu zenu katika dini na rafiki zenu tu..." [Qur'an, 33:5].

Kuhusu amri ya kumtaka Mtume amuoe Zainab, Qur'an inasema: "Wakumbushe ulipomwambia yule ambaye Allah amemneemesha (kwa kumpa Uislamu) na wewe ukamneemesha (kwa kumpa uungwana, naye ni Zaidu bin Haritha), 'Shikamana na mkeo na mche Mwenyezi Mungu' (usimuache). Na (wewe) ukaficha katika nafsi yako ambayo Allah alitaka kuyadhihirisha, (nayo ni umuowe wewe Zainab pindi Zaidu atakapomuacha, ili iondoke itikadi kwamba, mtoto wa kulea ni kama mtoto wa kumzaa), na ukawaogopa watu ilihali Allah ndiye ana haki Zaidi ya kuogopwa. Basi Zaidu alipomaliza haja yake kwa mwanamke huyo tulikuozesha wewe, ili isiwe tatizo (uzito) kwa Waislamu kuwaoa wake (waliokuwa) wa watoto wao wa kupanga wanapokuwa hawana haja nao tena (wakiwaacha). Na amri ya Allah hutekelezwa tu [Qur'an, 33:37].

***Kwa mrejesho, wasiliana na mwandishi kwa namba 0773181494***




AFYA YAKO

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Rika zote tuko hatarini, tuamke dhidi ya kisukari

Kila tarehe 14 Novemba dunia huadhimisha Siku ya Kisukari Duniani. Mwaka 2025 kaulimbiu ni "Diabetes across life stages" – ikikumbusha kuwa kisukari si ugonjwa wa wazee pekee, bali unaweza kumgusa mtoto, kijana, mwanamke mjamzito, mtu wa umri wa kazi na mzee.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya ya Tanzania, idadi ya wagonjwa wa kisukari waliofika kupata huduma iliongezeka kutoka 814,449 (Julai 2023–Juni 2024) hadi 863,942 (Julai 2024–Juni 2025). Ndani ya idadi hii, zaidi ya wanawake 200,000 walihudhuria kliniki wakiwa na kisukari, jambo linaloonyesha kuwa wanawake – wakiwemo wajawazito – ndio wanaoathirika zaidi.

Kisukari ni ugonjwa unaothiri namna mwili unavyotumia sukari kwenye damu (glucose). Kuna aina kuu nne: Kisukari aina ya kwanza hutokana na kinga ya mwili kuharibu seli za kongosho zinazozalisha insulini, na mara nyingi huanza utotoni au ujana, hivyo mgonjwa huhitaji sindano za insulini maisha yote. Aina ya pili hutokea pale seli za mwili zinapokuwa sugu kwa insulini au kongosho kushindwa kuitengeneza ya kutosha; hii inahusiana sana na unene uliokithiri, lishe duni na kutokufanya mazoezi. Pia kuna kisukari cha ujauzito kinachojitokeza wakati wa mimba, pamoja na hali ya "prediabetes" ambako sukari imeanza kupanda lakini bado haijafikia kiwango cha kisukari kamili – onyo la mapema kwamba maisha yanahitaji kubadilika.

Kidunia, makadirio yanaonyesha zaidi ya watu milioni 800 wanaishi na kisukari, na takribani nusu hawajui kama wana ugonjwa. Wengi wako katika nchi za kipato cha chini na cha kati ambako huduma na dawa zina changamoto za upatikanaji na gharama. Ndiyo maana WHO na nchi wanachama ziliweka malengo ya 2030: angalau asilimia 80 ya wenye kisukari kugunduliwa na kudhibiti sukari na shinikizo la damu, pamoja na kila mwenye kisukari aina ya kwanza kupata insulini na vifaa vya kujipima kwa bei nafuu.

Mwendo wa ugonjwa huu unabadilika kulingana na hatua za maisha. Kwa watoto na vijana, ongezeko la unene na kukaa muda mrefu bila mazoezi kunachochea kisukari aina ya pili mapema kuliko zamani. Kwa watu wa umri wa kazi, msongamano wa majukumu, vyakula vya haraka na kutokufanya mazoezi vinachangia hatari ya kupata kisukari na hivyo kuathiri uwezo kazini. Kwa wanawake wajawazito, kisukari cha ujauzito huongeza uwezekano wa matatizo ya mimba na kujifungua na huweka msingi wa kisukari aina ya pili baadaye kwa mama na mtoto. Kwa wazee, changamoto huongezeka kwa kuwa mara nyingi wanakabiliwa na magonjwa mengine sugu kama presha, magonjwa ya moyo na figo.

Mwaka huu WHO imezindua miongozo ya kimataifa ya usimamizi wa kisukari wakati wa ujauzito. Inasisitiza ushauri binafsishi wa lishe na mazoezi, uchunguzi wa mara kwa mara wa sukari kliniki na nyumbani, mpango maalumu wa dawa kulingana na aina ya kisukari, na huduma ya timu jumuishi kwa wajawazito wenye kisukari cha muda mrefu. Hili ni muhimu kwa Tanzania, ambako takwimu zinaonyesha wanawake ndio wanaongoza kwa kuhudhuria kliniki za kisukari.

Ili kuzuia madhara, ni muhimu kufahamu dalili. Mtu anaweza kuwa na kisukari bila kujua, lakini dalili za kawaida ni pamoja na kukojoa mara kwa mara hasa usiku, kiu isiyoisha, kula sana lakini kupungua uzito, uchovu, majeraha au vidonda vinavyochelewa kupona, kufa ganzi kwenye miguu na mikono na kuona ukungu. Dalili hizi zikijitokeza, hatua sahihi ni kwenda kupima mapema.

Kinga ya kisukari aina ya pili iko mikononi mwetu. Lishe yenye mboga, matunda, nafaka zisizokobolewa na kupunguza vyakula vya mafuta na sukari nyingi; kufanya mazoezi angalau dakika 30 kwa siku; kudhibiti uzito; kuacha tumbaku na kupunguza pombe – vyote vinapunguza hatari ya kupata ugonjwa na kuchelewesha madhara kwa walio ugua tayari. Uchunguzi wa mara kwa mara wa sukari, hasa kwa watu wenye historia ya kisukari kwenye familia au wenye unene kupindukia, unapaswa kuwa sehemu ya huduma za kawaida za afya kama kupima shinikizo la damu.

Kaulimbiu ya kitaifa mwaka huu inalenga mahali pa kazi. Waajiri wanahimizwa kuunda mazingira rafiki kwa wafanyakazi wenye kisukari: kuruhusu muda wa kupima sukari na kutumia dawa, kutoa elimu ya afya, kuweka chaguo la chakula bora kantini na kupunguza unyanyapaa. Mfanyakazi mwenye kisukari anapopewa msaada na si lawama, anaweza kuendelea kuchangia kwa ufanisi bila kuharibu afya yake.

Mwisho, vita dhidi ya kisukari si jukumu la wizara pekee. Ni jukumu la familia, jamii, viongozi wa kidini na waajiri. Kisukari si hukumu ya kifo, bali ugonjwa unaoweza kudhibitiwa na kuishi nao kwa ubora wa maisha.

IDARA YA DAAWA

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Jinsi ya kumfundisha mtoto kwenda haja

Kumfundisha mtoto kuacha nepi na kutumia choo ni hatua kubwa katika ukuaji wake. Wataalamu wanasema watoto wengi wako tayari kuanza kuanzia miezi 18 hadi miaka 4, lakini kila mtoto ana mwendo wake. Lengo si kumkimbiza, bali kumsaidia ajifunze taratibu bila shinikizo.

## Dalili za utayari

Kabla ya kuanza, angalia ishara fulani. Mtoto anayetembea vizuri na anaweza kukaa kwa muda mfupi anaweza kuwa karibu kuanza. Dalili nyingine ni kuwa na nepi kavu kwa zaidi ya saa mbili, kuonyesha kwa maneno au ishara akikojoa au akifanya haja kubwa, kuanza kuchukia nepi chafu na kujaribu kuivua, na uwezo wa kuvua na kuvaa suruali rahisi. Ukiona mwelekeo wa jumla wa dalili hizi, unaweza kuanza mafunzo.

## Vifaa unavyohitaji

Unaweza kuchagua kutumia poti au choo cha kawaida chenye kiti kidogo juu yake. Watoto wengine hujisikia salama zaidi kwenye poti iliyokaribishwa vizuri chumbani, wengine hupenda choo kwa sababu ndio wanachotumia watu wazima. Kama unatumia choo, weka kigoda cha kupandia na kiti kidogo kinachotoshea kwenye tundu la choo ili mtoto asihofie kuanguka.

Pia, nunua chupi au suruali za mazoezi (training pants) ambazo ni rahisi kuvua haraka. Mruhusu mtoto achague chupi anazozipenda; hatua hii humtia hamasa kuacha nepi. Ni vizuri pia kuwa na taulo ndogo za kufutia uchafu na sabuni ya mikono jirani na choo.

## Muandae mtoto taratibu

Kabla hujaanza rasmi, mtaje mara kwa mara maneno rahisi kama "kukojoa", "kuenda haja" au kauli kama "nataka chooni". Wakati wa kubadilisha nepi, muonyeshe kinyesi ukikimwaga kwenye poti au chooni na umwambie ndiko kunakostahili kwenda. Hii humsaidia kuunganisha haja na choo.

Hakikisha anakunywa maji ya kutosha na anakula vyakula vyenye nyuzi ili kuepuka kufunga choo, jambo ambalo linaweza kumfanya aogope kwenda haja kubwa. Mtoto mwenye maumivu anapokwenda haja anaweza kukataa kabisa kukaa kwenye poti.



## Kuanzisha mazoea ya choo

Chagua muda ambao familia haina misukosuko mikubwa kama kuhama nyumba, safari ndefu au kuanza shule ya awali. Siku ya kwanza ni vizuri ukae nyumbani. Anza kumpeleka mtoto kwenye poti au chooni asubuhi, kabla ya au baada ya chakula na kabla ya kulala.

Angalia ishara kama kukaa kimya ghafla, kukunja miguu, kusimama pembeni au kutoa gesi. Ukiwaona, mwalike kwa upole: "Twende kwenye poti." Usimlazimishe; mkalie dakika chache tu. Akijaribu, hata kama hakufanya chochote, msifu: "Umefanya vizuri kukaa kwenye poti."

Vaa nguo rahisi kuvua, mfano suruali za lastiki. Wakati wa mchana, tumia chupi badala ya nepi ili ajisikie anapolosha. Usiku unaweza kuendelea kutumia nepi au kitambaa maalumu kwenye godoro hadi uone anaamka asubuhi akiwa mkavu mara nyingi; hapo unaweza kujaribu kumuacha bila nepi usiku.

## Kutoka nje na safari

Mtoto akiwa bado kwenye mafunzo, jitahidi kujua choo kilipo kabla hamjaingia sokoni, msikitini au nyumbani kwa ndugu. Beba nguo za kubadilisha, chupi za ziada na mfuko wa plastiki kwa ajili ya nguo chafu. Kabla ya kutoka nyumbani au kabla ya kupanda gari, mkumbushe kwenda chooni ili kupunguza uwezekano wa ajali njiani.

## Usirudi nyuma

Ajali ni sehemu ya mafunzo. Mtoto akijikojolea au kujisaidia kwenye nguo, tulia, usimwandame wala kumdhalilisha. Msaidie kubadilisha nguo kwa utulivu na mwambie, "Sawa, tukijaribu tena tutatumia choo."

Watoto wengi husahau kwenda chooni wanapokuwa bize kucheza, hivyo mkumbushe mara kwa mara, hasa kabla ya kutoka nje au kabla ya shughuli mpya. Hakikisha poti au choo kinapatikana kwa urahisi.

Kuhusu usafi, msaidie kujifuta kutoka mbele kwenda nyuma (hasa kwa wasichana) ili kupunguza maambukizi ya njia ya mkojo. Wafundishe kuosha mikono kwa sabuni kila wanapotoka chooni.

## Mtazamo wa mzazi ni muhimu

Mafanikio ya mafunzo haya yanategemea zaidi mtazamo wa mzazi kuliko umri halisi wa mtoto. Zingatia kanuni kadhaa: kuwa thabiti (usiende kurudi kwenye nepi bila sababu za msingi), kuwa mvumilivu, kuwa mtulivu na usiseme maneno ya kumkatisha tamaa. Epuka kumlazimisha, kumtishia au kumchapa. Badala ya viboko na ahadi nyingi za zawadi, tumia pongezi ndogo za kila siku, tabasamu na kukumbatia.

Wazazi wengi hupata presha kutoka kwa watu wanaosema "subiri bado mdogo" au "mtoto wangu alijifundisha mwenyewe".

Kumbuka, wewe ndiye unayemvalisha nepi na kutunza usafi wake; una haki pia ya kumfunza kuiacha kwa utaratibu, mapema au baadaye kadiri mnavyoweza. Kila mtoto atafika tu, akiwa na msaada wa mzazi mwenye upendo, uthabiti na matumaini.




# Nini kinafanya tufanye maamuzi tunayofanya?

**Kila siku tunachagua: kuvaa nini, kula nini, tumtumie nani ujumbe, kutumia au kutotumia hela, kubaki kazini au kuondoka.**
**Mara nyingi tunaamini tunatumia "akili ya kawaida" tu, lakini kwa ndani maamuzi yetu yanaongozwa na mchanganyiko wa hisia, fikra, kumbukumbu, mitazamo potofu na ushawishi wa wengine. Kuelewa nguvu hizi hutusaidia kuelewa kwa nini tunachagua tunachochagua – na jinsi ya kuboresha maamuzi yetu.**

### Mosi, mifumo miwili

Maamuzi yetu yanaendeshwa na mifumo miwili ya kufikiri. Wataalamu wa saikolojia wanaieleza kama mfumo wa haraka na wa polepole. Mfumo wa haraka ni wa hisia na hali ya "kubetua" – unafanya kazi bila kutafakari sana, unategemea uzoefu wa nyuma na hisia za papo kwa papo.

Mfumo wa polepole ni wa uchambuzi – unahitaji muda na utulivu; unalinganisha faida na hasara, unaangalia matokeo ya muda mrefu kabla ya kuamua. Changamoto ni kwamba mara nyingi tunategemea mfumo wa haraka hata pale ambapo tungehitaji kutulia na kutafakari kwa kina.

### Pili, hisia zina nguvu zaidi

Hisia zina mchango mkubwa kuliko tunavyopenda kukubali. Hofu inaweza kutufanya tukatae fursa nzuri kwa sababu tu "inaonekana hatari"; furaha na msisimko vinaweza kutusukuma kununua kitu kisichokuwa kwenye bajeti; aibu inaweza kutufanya tukubaliane na uamuzi wa kundi ili tusionekane wa ajabu. Hata maamuzi ya kibiashara na kazi – kama kubadili ajira au kuwekeza pesa – huwa hayaguswi na takwimu pekee, bali na hisia zetu kuhusu usalama na heshima.

### Tatu, upendeleo wa kiakili

Tunakosea mara nyingi kwa sababu ya upendeleo wa kiakili (cognitive biases) ambao hatuuoni. Kuna ule upendeleo wa kutafuta taarifa zinazothibitisha kile tunachoamini tayari; tukishaamini bidhaa fulani ni "bora", tunapuuzia maoni hasi kuhusu bidhaa hiyo. Kuna tabia ya kuogopa kupoteza zaidi ya tunavyofurahia kupata; tunaweza kushikilia biashara isiyoleta faida kwa sababu "tumeshawekeza sana", badala ya kukubali kupoteza kidogo na kubadili mwelekeo. Pia tunapenda hali tuliyoizoea; kubaki kwenye kazi isiyoturidhisha huonekana "salama" kuliko kujaribu fursa mpya.

### Nne, matarajio ya jamii

Maamuzi yetu yanaathiriwa sana na watu waliotuzunguka na matarajio ya jamii. Tunapouona umati ukikimbilia bidhaa fulani mtandaoni, akili zetu zinatuambia "kama wote wanapenda, basi ni sahihi." Ndiyo maana tathmini za wateja, maoni ya marafiki, au mtazamo wa familia kuhusu kazi, ndoa au masomo vinaweza kutusukuma kuchagua jambo ambalo si lazima lingeendana na ndani ya mioyo yetu. Mara nyingi hatutaki tu kufanya uamuzi sahihi, tunataka pia kukubalika na kundi.

Tano, mazingira na namna chaguo yanavyowasilishwa vina ushawishi wa siri. Bei ikionyeshwa kama "punguzo la asilimia 50" tunaiona ni nafuu zaidi kuliko bei ileile iliyoandikwa kwa namba bila maelezo. Maneno, picha, muziki wa duka au mwanga wa chumba vinaweza kutuandaa kiakili kuchagua kwa njia fulani bila kujua. Kadhalika, uchovu wa akili baada ya maamuzi mengi siku nzima hutusukuma kuchagua kilicho rahisi na cha haraka, siyo kile kilicho bora.

### Sita, maono (intuition)

uzoefu na kumbukumbu zetu huunda kile tunachokiita "hali ya tumbo" au intuition. Mara nyingi uamuzi wa haraka unaoonekana kama hisia tu unakuwa umejengwa juu ya miaka ya mifumo tuliyoiona na kuihifadhi kwenye ubongo. Mwalimu mwenye uzoefu anaweza "kuhisi" darasa haliko sawa, au mfanyabiashara kuhisi mteja hatalipa, hata bila hoja nyingi za mezani. Intuition inaweza kutusaidia pale ambapo tumepata muda wa kujifunza na kupata mrejesho mara kwa mara, lakini kwenye mazingira mapya kabisa kutegemea hisia peke yake kunaweza kutupotosha.

### Saba, vipi tuboreshe?

Tukisha kuelewa kwamba maamuzi yetu hayazaliwi tu kwenye karatasi za mantiki, tunapata nafasi ya kuyaboresha. Hatua muhimu ni kujitambua: kutambua ninapokuwa nimechoka, nina hofu au nimekasirika, na hivyo kuahirisha maamuzi makubwa hadi nitakapokuwa mtulivu. Pia tunaweza kupunguza ushawishi wa upendeleo wa kiakili kwa kujilazimisha kuangalia upande mwingine wa hoja: je, kuna taarifa gani inayopingana na ninachotaka kuamini? Mwisho ni kutafuta mtazamo tofauti kutoka kwa watu wanaotofautiana nasi – si wale wanaotusemea "ndiyo" tu.

Nimalize kwa kusema tunapojua nini kinaendesha maamuzi yetu, tunaweza kuunganisha vizuri kati ya hisia na hoja. Si sahihi kuamini kwamba akili ya hisia ni mbaya na ya mantiki ndiyo nzuri pekee; zote mbili zinahitajika. Changamoto ni kuzisikiliza kwa uwiano: kutumia hisia kutuonyesha kilicho muhimu kwetu, na kutumia hoja kutuchanganulia njia bora ya kukifikia. Hapo ndipo maamuzi yetu yanapoanza kuakisi siyo tu msukumo wa dakika hii, bali maisha tuliyoamua kuyaishi.



# Makosa wanayofanya wajasiriamali chipukizi – na utayakwepaje

Kuanza biashara ni hatua kubwa lakini pia kuna hatari nyingi zisizoonekana. Bila kuelewa makosa ya kawaida ya wajasiriamali chipukizi, mtu anaweza kujikuta amechoka, amepoteza fedha na hata kuichukia biashara kabla haijakua.Makala hii inaeleza makosa yanayojirudia mara nyingi, na unavyoweza kuyaepuka ufanikiwe.

## Mosi, kukosa utafiti

Wazo zuri pekee halitoshi kama huna mpango wa biashara unaoainisha unamuuzia nani, anahitaji nini, yuko wapi na atalipa kiasi gani. Wengi hufungua duka kwa kufuata mkumbo tu, bila kuelewa ushindani uliopo, gharama za uendeshaji na njia halisi ya kupata faida.

Mpango rahisi unaoonyesha mteja unayemlenga, tatizo unalotatua, gharama, bei na njia za kumfikia unasaidia kuzuia biashara kugeuka shimo la kutupia fedha.

## Pili, "Nitaanza niki ..."

Wajasiriamali wengi husubiri "wakati sahihi" kwa kutafuta ukamilifu. Wanasema, "nikipata mtaji zaidi", "nikimaliza logo", "nikipata ofisi nzuri", ndipo waanze. Muda unakwenda, soko linabadilika, na ujasiri unapungua.

Ukweli ni kwamba hutaweza kujua kila kitu kabla ya kuanza. Ni bora kuanza kidogokidogo huku ukisikilizia mrejesho wa wateja na kuboresha ukiwa njiani kuliko kung'ang'ania mpango wa karatasi usiofika sokoni.

## Tatu, kuiga bila nyongeza ya ubunifu

Unaona mtu anauza mtandaoni na anafanikiwa, unakimbilia kuuza kitu kilekile kwa mtindo uleule na bei zilezile. Unasahau kwamba historia yake, mtandao wake, wateja wake na muda aliotumia kujijenga ni tofauti na wako.

Kila soko linahitaji "ladha" yako ya kipekee. Badala ya kunakili, jifunze kinachofanya wengine wafanikiwe, kisha ujiulize: mimi natofautishaje huduma yangu au bidhaa yangu kwa kundi ninalolilenga?

## Nne, kutomsikiliza mteja

Mteja anaweza penda bidhaa yako lakini nawe unahiaji kujua safari ya mteja kuanzia anapokuona, kununua, kutumia bidhaa hadi kurudi tena. Kwa kutojua hilo na kuwahudumia ipasavyo, wateja hawarudi, hawapendekezi bidhaa yako kwa wengine, na maoni hasi mtandaoni yanazidi.

Suluhisho ni kumfikiria mteja katika kila hatua: urahisi wa kuwasiliana, kasi ya kujibiwa, ubora wa kifungashio, ufikaji wa bidhaa kwa wakati na huduma baada ya mauzo. Uliza mara kwa mara, "Nini nikiboreshe?" na uchukulia maoni yao kwa umakini.

## Tano, kupambana peke yako

Ni kweli hii ni ndoto yako, lakini haimaanishi uwe mtaalamu wa masoko, fedha, mauzo, bidhaa na teknolojia kwa wakati mmoja. Itafika hatua utachoka, utachelewa kufanya maamuzi muhimu na kupoteza fursa. Ni busara kutafuta ushauri kutoka kwa waliokutangulia, kutumia marafiki au ndugu walio na ujuzi maalumu, au hata kumleta mfanyakazi au mwanafunzi kufanya sehemu ya kazi ili uwe huru kushughulikia maamuzi makubwa.

## Siti, ushirika usioleweka

Kuna watu wanagawana umiliki wa biashara "kwa maneno" tu, bila kuandikiana idadi ya hisa za kila mmoja, wajibu, muda wa kujitolea na mgawanyo wa faida. Baadaye mmoja anafanya kazi zaidi, mwingine hashiriki, lakini bado anataka haki sawa.

Ni muhimu kujiuliza: atamiliki hisa asilimia ngapi, atafanya kwani haya yasipowekwa bayana mapema hupelekea migogoro itakayovunja biashara yenye uwezekano wa kufanikiwa. Mkataba rahisi wa maandishi unaweza kuokoa urafiki na biashara yako.

## Saba, kutowekeza kwa watu kwa faida ya muda mrefu

Kosa jingine kubwa ni kuchukulia mahusiano kama miamala ya haraka tu badala ya uwekezaji wa muda mrefu. Baadhi ya wajasiriamali wakikutana na mtu mpya, wanalazimisha kumuuuzia mara moja bila kujenga imani.

Mtazamo huu unafunga milango mingi. Unapowasikiliza watu, kuwauliza maswali, kuelewa hadithi zao na kutafuta namna ya kuongeza thamani kabla ya kudai chochote, unaacha alama nzuri mioyoni mwao. Biashara inakumbukwa kwa hisia ulizowaachia watu, si kwa hotuba yako ndefu ya mauzo.

## Nane, maamuzi ya kihisia

Wengi huangukia kwenye mtego wa kupenda wazo lao kupita kiasi na kukosa kubadilika. Wanapewa mrejesho kwamba soko halihitaji kile wanachouza au kwamba aina ya mteja waliyemlenga si sahihi, lakini wanakataa kusikia.

Wanadai "wengine hawaelewi", ilhali takwimu na matokeo ya mauzo yanaonyesha wazi kuwa mwelekeo si mzuri. Ujasiriamali unahitaji moyo wa kubadilisha mwelekeo ikiwemo mpaka bidhaa ipate nafasi yake sahihi sokoni.

## Tisa, kukata tamaa

Changamoto kama kukataliwa na wateja, maoni ya kejeli na mauzo ya kusuasua zinawafanya baadhi ya wajasiriamali kufunga biashara haraka. Wanasahau kwamba kila safari kubwa imejaa mapindo, vizingiti na majaribu.

Badala ya kupima mafanikio kwa faida ya siku chache za mwanzo, pima ulichojifunza, mitandao uliyojenga, ujasiri ulioongezeka na mabadiliko uliyofanya kwenye mpango wako. Anayeendelea kusonga mbele, akijifunza kutokana na makosa, ndiye anayebaki uwanjani hadi aanze kuona matunda.